# Nipashe

**Ijumaa Oktoba 27, 2023** Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581476

MWANGA WA JAMII



0745 700710 LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com




UKURASA 21

**MANÉ KUNUNUA KLABU UFARANSA**

MAKONDA ASEMA...

# Sitolipa kisasi

• **Awapa** angalizo mawaziri, wakuu wa mikoa; wataalamu sayansi ya siasa wakuna vichwa... *Endelea ukurasa 2*



Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi na Uenezi, Paul Makonda, akiendesha pikipiki, wakati akiwasili katika mapokezi yake kwenye Ofisi Ndogo za Makao Makuu ya chama hicho, Lumumba, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Bodi ya Mikopo kunasa wakwepa deni wakitumia S/Mitaa

UKURASA 2

UKURASA WA 7

**Mke** wa Bilionea Msuya: Nilipelekwa porini, wakanihoji wakiwa na bastola



UKURASA WA 17

**Dk.** Mwinyi atoa tahadhari kasi ya ongezeko la watu



UKURASA WA 19

**Watanzania** wawili watoweka Israel, Ufaransa yaonya kinachojiri Gaza



## Mpango ang'aka mchezo mchafu kuzuia ujenzi viwanda vya dawa

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA YATAKA KUJIIMARISHA KILELENI LEO** UK.24

**KATUNI** UK.6

# Makonda asema hatolipa kisasi

Na Jenifer Gilla

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Paul Makonda, amesema hana mpango wa kulipiza kisasi kwa mtu yeyote kama baadhi ya watu wanavyofikiri, bali atafanya kazi aliyokabidhiwa.

Vilevile, amewataka mawaziri, wakuu wa mikoa na watendaji wa serikalini kuwajibika katika majukumu na kutenda haki kwa wananchi kwa kuwa chama hicho hakitosita kumchukulia hatua kiongozi asiyefanya kazi kikamilifu.

Makonda alitangaza hayo jana katika hafla ya mapokezi yake iliyofanyika ofisi ndogo za chama hicho Lumumba jijini Dar es Salaam. Ni baada ya kuteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kushika wadhifa huo Oktoba 22 mwaka huu.

Aliwasili katika ofisi hizo saa tano asubuhi jana akiwa katika pikipiki na kulakiwa na mamia ya watu, akianzia katika ofisi kuu ambako alikabidhiwa ofisi kisha kwenda ofisi ndogo kwa ajili ya hafla fupi.

Akizungumza na umati uliokuwa umemzunguka, Makonda alisema tangu alipoteuliwa, aliona katika mitandao ya kijamii maoni ya baadhi ya watu yakizungumzia kuwa atalipa kisasi huku baadhi wakiwataja wanaodhani atawashughulikia, jambo alilosisitiza halitatokea.

Alisema asije akatokea mtu yeyote akadhani kuwa atashughuliwa kwa kufikiri kuwa amemtendea vibaya, asiwe na hofu kwa kuwa anaamini kuwa Mungu amemtumia kumsaidia kumjua zaidi, kuwa mnyenyekevu zaidi na kumwandaa kwa kazi kubwa zaidi iliyoko mbele yake.

Alisema mwenyekiti wa chama hicho, Rais Samia na viongozi wakuu hawakumteua na kumpitisha ili aje alipe kisasi, kujitutumua na kuonesha mabavu dhidi waliomtendea mabaya, bali kufanya kazi moja ya itikadi na uenezi wa chama hicho.

"Ninaomba niseme haya mbele ya hadhara hii na mbele ya Watanzania, wapenzi wa CCM, wakereketwa na mbele ya Mungu, mimi sina kisasi kwa mtu yeyote, na asiwapo mtu yeyote akafikiri nipo hapa kumkandamiza ," alisema.

### VIONGOZI SERIKALINI

Makonda, aliyewahi kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, alitoa angalizo kwa mawaziri, wakuu wa mikoa na watendaji wa serikali kuwa pale watapobainika kuwa hawajafanya kazi yao kikamilifu na kutenda haki kwa wananchi, chama hicho hakitosita kuchukua hatua.

Alisema hatokuwa tayari kuwa msemaji wa chama ambacho kimepewa dhamana, lakini aseme uongo pale ambapo viongozi hao watashindwa kumsaidia kiongozi mkuu wa nchi.



"Kila kiongozi wa serikali atabeba msalaba wake mwenyewe, sijahifadhiwa miaka mitatu na miezi mitatu kusema uongo, sijateuliwa na CCM kusema uongo. Na katika kiapo chetu ipo wazi - fitina, uongo, uzushi si sehemu ya CCM," alisema.

Aliwaomba wanachama wote wa chama hicho wadumishe upendo ili kujenga uhusiano na kuimarisha umoja wa kitaifa kama anavyofanya Mwenyekiti wa chama hicho, Rais Samia.

Makonda pia alirusha vijembe vya kisiasa kwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akiwataka viongozi wa mamlaka ya anga kumpa kibali mwanasiasa huyo ili aendelee kutumia helkopta katika ziara zake mikoani na kama hana mafuta, Rais Samia atamchangia.

Alidai CCM haitishwi na ziara zake kwa kuwa inaitekeleza vizuri ilani yake ya uchaguzi. Pia alisdai vyama vya upinzani kuhisi kuwa CCM inalitumia Jeshi la Polisi kuzuia mihadhara yao si kweli na haoni haja chama hicho kufanya mambo hayo kwa kuwa kina uwezo wa kuwashinda katika uchaguzi kwa kuwa kinatekeleza vilivyo ilani yake.

"Akiruka angani tutamfuata, akienda nchi kavu tutamfuata, akienda kwenye boti tutamfuata, atapigwa kila kona kwa sababu moja tu - hoja, vigezo na ilani ya CCM haina shaka," alitamba Makonda.

Alimshukuru Rais na Kamati Kuu ya chama hicho kwa kumwamini na kumpa wadhifa huo na kuahidi kufanya kazi hiyo kwa uaminifu na uadilifu huku akimwomba Mungu ampe hekima, busara na maarifa ili asiwaangushe waliomteua.

Vilevile, aliwaomba watendaji wa chama hicho kumfundisha, kumwelekeza na kumshauri kwa uaminifu na kumpa taarifa zenye ukweli ili zimsaidie kufanya uamuzi mzuri. Taarifa zikiwa si za kweli, husababisha mtu kufanya uamuzi mbovu.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Idara ya Oganaizesheni, Issa Gavu, alisema mabadiliko yanayofanywa katika chama hicho yanalenga kujenga safu imara ili kujihakikishia ushindi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwakani na Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.

Alisema viongozi wa chama hicho watafanya kila walilojaaliwa kuhakikisha chama chao kinapata ushindi katika uchaguzi huo.

Wakati akimkabidhi Makonda ofisi, aliyekuwa Katibu wa NEC Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema, alimshauri kukiendeleza chama hicho na kuhakikisha kinapata ushindi katika uchaguzi ujao.

### WATAALAMU SIASA

Mwanadiplomasia na mchambuzi wa siasa, Hamduni Maliseli, alipotafutwa na mwandishi kuzungumzia kauli za Makonda za jana, alisema kitendo chake cha kuwakumbusha wajibu wao viongozi wa serikali ni sahihi kwa kuwa ndiyo kazi yake kubwa. Katibu wa Itikadi na Uenezi ana wajibu wa kuangalia utendaji kazi wa viongozi hao na kuitaarifu serikali.

Alisema viongozi wa chama kazi yao kuu ni kuangalia mienendo ya wawakilishi waliopewa dhamana na chama kuiongoza nchi na kukemea pale wanapokwenda kinyume na kutoa taarifa kwa wanachama ili kama hawafai waondolewe na kuwekwa wengine.

"Katibu wa uenezi na Itikadi ni jicho la chama kwa serikali, akikosa meno lazima serikali itabweteka. Sasa huyu kazi yake ni kupiga kelele na kuiambia serikali kwamba kile chombo mlichokiweka humu hakiendi sawasawa. Na kwa bahati nzuri safari hii wamepata mbwekaji kwelikweli," alisema.

Kuhusu kiongozi huyo kusema kuwa hatolipa kisasi, mtaalamu huyo wa sayansi ya siasa alisema "ni mapema sana kuthibitisha ukweli wa jambo hilo kwa kuwa aliyezungumza ni binadamu, hivyo jamii impe muda wa miaka kadhaa ili kuthibisha ukweli wa kauli hiyo".

Mchambuzi wa Siasa, Luaga Kizoka alisema Makonda ni kiongozi anayeelewa namna siasa za kisasa zinavyokwenda, hivyo hawezi kuweka chuki na mtu, bali kuitumikia nchi kupitia wadhifa aliopewa katika chama hicho.

Pia alisema ni jukumu la Makonda kuwakumbusha viongozi wa serikali kuacha siasa na kufanya kazi kulingana na dhamana waliyopewa ili wakidhi mahitaji na kiu ya wananchi.

## Bodi ya Mikopo kunasa wakwepa deni wakitumia serikali za mitaa

Na Gwamaka Alipipi

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imesema inatarajia kuwatumia viongozi wa serikali za mitaa na vijiji kuwabaini wanufaika ambao wamekaidi kurejesha mikopo.

Pia inatarajia kuanzisha kampeni ya 'Fichua' itakayowawezesha wananchi kutoa taarifa za wanufaika wasiojitokeza kwa hiari kufanya marejesho ya mikopo.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi hiyo, Abdul-Razaq Badru, alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano uliohusisha wahariri, waandishi wa habari na maofisa wa HESLB, ukilenga kutoa taarifa na ufafanuzi wa masuala mbalimbali kuhusu taasisi hiyo.

Kwa mujibu wa HESLB, mkopo huanza kulipwa inapomalizika miezi 24 baada ya kuhitimu masomo ya elimu ya juu au baada ya kusitisha masomo kwa sababu yoyote ile.

Kwa wanufaika waajiriwa, hukatwa asilimia 15 ya mshahara wa kila mwezi. Mnufaika aliyejiajiri anapaswa kurejesha kiwango cha chini cha Sh. 100,000 kila mwezi. Njia ya kuhusisha serikali za mitaa na vijiji itasaidia kuwabaini wanufaika walipo na kurejesha mkopo huo.

Akizungumzia utoaji mikopo, Badru alisema mwaka 2020/21 walitoa Sh. bilioni 464 kwa wanafunzi 149,508, mwaka 2021/22 walitoa Sh. bilioni 570 kwa wanafunzi 177,892, mwaka 2022/23 walitoa Sh. bilioni 654 kwa wanafunzi 198,105 na mwaka 2023/24 wametoa Sh. bilioni 786 kwa wanafunzi 220,376.

Badru alisema: "Kwa mwaka 2023/24, Sh. bilioni 731 zimetengwa kwa ajili ya kusomesha wanafunzi 220,376 wakiwamo wanafunzi wa mwaka wa kwanza 75,000 watakaojiunga na vyuo kwa ajili ya masomo ya shahada ya kwanza. Pamoja na kunufaisha wanafunzi 145,376 wanaoendelea na masomo."

Kuhusu ufadhili wa masomo kupitia programu ya Rais Samia, "Samia Scholarship", alisema Sh. bilioni 6.7 zimetengwa kwa ajili ya wanufaika 1,276 wakiwamo wanafunzi 640 wapya.

Vilevile, alisema Sh. bilioni 48 zimetengwa kwa ajili ya kuwawezesha wanafunzi wa stashahada 8,000, akitaja fani za kipaumbele kuwa ni afya na sayansi shirikishi, elimu, usafiri na usafirishaji, uhandisi na nishati, madini na sayansi ya ardhi, kilimo na mifugo.

Kuhusu urejeshaji wa mikopo, Badru alisema katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2020 hadi 2023 Sh. bilioni 530 zimekusanywa kati ya malengo ya ukusanyaji Sh. bilioni 565.

"Kuanzia mwaka 1994 hadi sasa tumeshatoa mikopo kwa wanufaika 754,000 na tumetoa Sh. trilioni 7.2, tumeshakusanya Sh.trioni 1.34, marejesho yaliyoiva ni Sh. trilioni 2.1 kutoka kwa wanufaika 235,498, kiasi ambacho hakijakusanywa ni Sh. bilioni 758 kati ya kiwango cha marejesho yaliyoiva," alisema Badru.

Kuhusu malengo waliyonayo, Badru alisema wamejipanga kukamilisha ushirikiano wa kimkakati na NSSF, TRA, PSSSF, BRELA ili kubadilisha taarifa.

Badru alisema pia wanatarajia kuboresha huduma za urejeshaji mikopo kidijitali ili kurahisisha wanufaika kulipa popote na kiasi chochote kwa urahisi.

Alitaja lengo lingine ni kuhamasisha kuchangamkia fursa za mikopo kwa stashahada za kipaumbele zenye ajira, kuendelea kutoa elimu ya uombaji sahihi kupitia kampeni ya #WeweNDOFuture.

Lengo lingine ni kufanya mapitio ya kina ya muundo na utendaji kazi wa HESLB na kufanya mapitio ya king'amua uwezo, pamoja na uhamasishaji wadau kujiunga na GovESB chini ya e-GA.

## HABARI KITAIFA



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango akisikiliza maelezo kutoka kwa Mkuu wa Mradi wa Kiwanda cha Mipira ya Mikono (Gloves) cha MSD, Selwa Hamid kuhusu maendeleo ya kiwanda alipotembelea na kukagua shughuli mbalimbali zinazofanyika kiwandani hapo, eneo la Idofi, Makambako mkoani Njombe jana. **PICHA: OMR**

# Mpango ang'aka mchezo mchafu kuzuia ujenzi viwanda vya dawa

**Na Mariam Mziwanda**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema serikali inatambua vita iliyopo katika ujenzi wa viwanda vya dawa nchini, lakini uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan hauna wa kuukwamisha.

Amesema kwa sasa serikali inaagiza dawa kwa asilimia 80 na vifaa tiba kwa asilimia 90 kutoka nje ya nchi, hali inayosababisha uhaba wa vifaa na gharama kubwa za uagizaji wa vifaa vya afya.

Pia, ametoa maagizo saba kwa Wizara ya Afya na Bohari ya Dawa (MSD) ikiwamo kuanza kuzalisha majitiba, vitendanishi vya maabara na watumishi kuchunguzwa ili wasitumiwe na wafanyabiashara kuhujumu juhudi za serikali.

Akizungumza jana mkoani Njombe, wakati wa uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa kiwanda cha mipira ya mikono (Gloves) kinachosimamiwa na Bohari ya Dawa (MSD), Makamu wa Rais Dk. Mpango alisema serikali inatambua vita iliyopo katika ujenzi wa viwanda hivyo vya dawa.

Alisema, Rais Samia ameamua viwanda hivyo vitajengwa kwa gharama yoyote kwa kuwa nchi ina uhaba wa dawa na vifaa tiba.

"Ujenzi wa viwanda hivi umelenga kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba, kupunguza matumizi ya fedha za kigeni, uhaba wa dawa, gharama kubwa kuagiza bidhaa hizo na kutoa ajira," alisema.

"Kuwapo wa kiwanda hiki ni muhimu sana kwa ajili ya mahitaji ya ndani na nje ya nchi wakati wa Corona tulihangaika sana matumizi ya gloves ni makubwa kiwanda hiki ni mkombozi hivyo lengo la Rais Dk. Samia lazima lifikiwe," alisisitiza.

Dk. Mpango alisema, wapo katika mkakati wa kuiongezea mtaji MSD ili kujenga viwanda na maghala na kuongeza upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.

"Nataka uzalishaji wa kiwanda uanze mara moja Januari mosi mwaka 2024 na kiwanda hiki hakitoki hapa kitabaki, kitazalisha niwaagize MSD ongezeni uzalishaji mwingine wa majitiba na vitendanishi na kampuni Tanzu ya MSD zingatieni misingi ya kibiashara na watumishi zingatieni uzalendo,"alisema.

Dk. Mpango alisema, ameteta na Rais Dk. Samia akiwa katika tukio hilo na kuagiza Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kupitia Wakala wa Barabara Vijijini wafanye tathmini ya ujenzi wa barabara ya kwenda katika kiwanda hicho ambayo inahitaji Sh. bilioni 1.4 ili ijengwe kwa kiwango cha lami.

"Hiyo ndio salamu ya Rais mimenong'ona naye hapa hapa kasema hashindwi kujenga barabara hii, hivyo nawapa wiki mbili TAMISEMI malizeni tathmini ujenzi uanze," alisema.

Aliiagiza Wizara ya Fedha kuhakikisha fedha zilizotengwa kupunguza deni la MSD zitolewe haraka iwezekanavyo ili wasiendelee kulialia.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Molel alisema, wizara inatambua mapinduzi makubwa yanayofanywa na Rais Dk. Samia na serikali yake katika kuleta mapinduzi sekta ya viwanda hususani vya dawa.

Kutokana na hali hiyo aliahidi wizara itahakikisha hakuna kinachokwama na kiwanda hicho kitaanza uzalishaji licha ya vita kubwa iliyopo.

Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Mavere Tukai, alisema kiwanda hicho kimeanza uzalishaji wa awali na kinatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka huu.

Alisisitiza kiwanda hicho kitasaidia kukuza uchumi na ndani ya miaka minane kitarudisha faida na kwa mwaka wa kwanza itakuwa ni zaidi ya Shilingi bilioni moja na ajira 200 kwa moja kwa moja na za muda.

Alisema kiwanda cha mipira ya mikono (gloves) Idofi hadi kikamilike kitagharimu sh. bilioni 22.5, na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha mipira ya mikono 20,000 kwa saa sawa na jozi (pairs) 10,000.

# ACT yatamba kushinda Jimbo la Mtambwe

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT -Wazalendo, Othman Masoud, amesema mgombea wa Chama hicho, Dk. Muhammed Ali Suleiman anakidhi kuwa mwakilishi wa Jimbo la Mtambwe.

Alisema hivi sasa kuna ufisadi mkubwa kwenye ununuzi serikalini na mgombea huyo ni mtaalamu wa ununuzi ambaye ataenda kuwasemea Wazanzibari katika Baraza la Wawakilishi.

Alisema katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, ACT ilinyang'anywa kila kitu na kubaki na wawakilishi wanne katika majimbo 50 ya uchaguzi Unguja na Pemba.

Othman ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais, alisema wanatakachokifanya Oktoba 28, mwaka huu katika uchaguzi huo mdogo, wanakwenda kuiambia dunia kwa kupaza sauti zao kuwa hawataki na hawakubali nchi kuongozwa kwa ufisadi na unafiki.

"Zanzibar sio ya kuwa na ufukara huu uliopo, na baadhi ya watu wanatumia juhudi kubwa ya ghilba na dhuluma," alisema.

Alisema katika Sheria ya Rushwa hakuna kosa kubwa kama mtu kupewa ofisi ya umma kuitumia vibaya kwa maslahi yake binafsi au kisiasa, lakini kuna mtu kapewa mamlaka hayo ya kutumikia wananchi, lakini anaitumia vibaya.

Alisema lazima kitendo hicho kikomeshwe maana ni kosa kubwa la jinai la uhujumu uchumi na lazima ifike mahala nchi iendeshwe kwa ustaarabu.

Alisema juhudi za Maalim Seif ilikuwa ni kusimamia maridhiano ya nchi, lakini juhudi hizo hazifanyiwi kazi na ndio maana kuna vitendo vya dhuluma.

Othman aliwataka wananchi wa Jimbo la Mtambwe kumchagua mgombea wa chama hicho ili aende kukomesha ufisadi na kuwaletea maendeleo wananchi wa jimbo hilo. Mjumbe wa kamati kuu ya chama hicho, Ismail Jussa, alisema aliyefungua dimba kuwa mwakilishi wa jimbo hilo mwaka 1985 ni marehemu Maalim Seif Sharif Hamad.

Jussa alisema Pemba haifundishwi siasa na Zanzibar haiwezi kusonga mbele bila ya mamlaka kamili.

Alisema wazanzibari sio limbukeni wa shule za ghorofa na zilikuwapo tangu miaka 100 iliyopita, Wazanzibari kwenye siasa hawadanganyiki.

Mkurugenzi wa oganaizesheni wa chama hicho, Omar Shehe, alisema sheria itakayotumika ya uchaguzi huo mdogo ya Tume ya Uchaguzi ni ya mwaka 2020 ambayo iliwanyima fursa ya kushiriki uchaguzi.

Mgombea uwakilishi wa jimbo hilo, Dk. Muhammed Ali Suleiman, alisema siasa za mageuzi zilianzia katika jimbo hilo na hadi sasa hakuna maendeleo.

Aliwataka wananchi kuwakopesha dhamana zao kwa kumpigia kura za ndio zitakazomwezesha kuwa mwakilishi ili kuwalipa maendeleo.

Uchaguzi mdogo wa jimbo hilo unatarajiwa kufanyika kesho na unatokana na kifo cha aliyekuwa mwakilishi wa Jimbo hilo, Habib Muhammed.


CHAMA CHA WALIMU TANZANIA
CWT
WAJIBU NA HAKI

## Invitation for Tenders

### Tender No. TTU/T/C/MWNZ/2023 for Supply of Teachers' Day T-shirts and Caps at Mwanza Region

**Date: October 27, 2023**

1. This Invitation for Tenders follows Tanzania Teachers' Union, which appears in Tanzania Teachers' Union financial regulations 3rd Edition of 2018.
2. Tanzania Teachers' Union has set aside funds for supply of Teachers' Day T-shirts and Caps at Mwanza Region during the financial year December 2023.
3. Tanzania Teachers' Union now invites tenders from eligible Supplier to Supply Teachers' Day T-shirts and Caps at Mwanza Region on December 2023.
4. Tendering will be conducted through the National Competitive Tendering method specified in Tanzania Teachers' Union Financial Regulations 3rd edition of 2018.
5. Interested eligible Tenderers may obtain, inspect the tendering document physically at Tanzania Teachers' Union, and pay tender participation of non-refundable fee of Tanzania Shillings 100,000. Payment is performed through bank via account National Microfinance Bank (NMB) 20101300312 Name Tanzania Teachers' Union and collect set of Tendering Documents manually from at Tanzania Teachers' Union Head quarter office, Jamhuri Stadium from 8:00 AM to 10:00 PM (Monday to Friday).
6. All Tenders must be physically submitted in the proper format, at or before 13/11/2023, 09:59AM. Tenders will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Tenderers' representatives who choose to attend at TTU- Head quarter office, ground floor meeting room, Box 3077, Jamhuri Stadium Dodoma.

General Secretary
Tanzania Teachers' Union-TTU
P.O.BOX 3077
DODOMA

THE SECRETARY GENERAL
TANZANIA TEACHERS' UNION (TTU)
DODOMA - HEADQUARTERS.

TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

www.tcbbank.co.tz

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA(HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

# TANZANIA COMMERCIAL BANK PLC

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | | Robo Mwaka /Mwaka wa sasa 30.09.2023 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30.06.2023 |
|---|---|---|---|---|
| A. | | **MALI** | | |
| | 1 | Fedha Taslimu | 63,280 | 53,615 |
| | 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 89,759 | 13,634 |
| | 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 146,464 | 143,237 |
| | 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 112,440 | 99,319 |
| | 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 12 | 512 |
| | 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| | 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| | 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 10,281 | 117,459 |
| | 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| | 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 898,894 | 837,161 |
| | 12 | Mali Nyingine | 47,204 | 41,797 |
| | 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| | 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| | 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 19,695 | 20,593 |
| | **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,388,029** | **1,327,327** |
| B | | **DHIMA** | | |
| | 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 0 |
| | 18 | Amana za Wateja | 910,090 | 870,917 |
| | 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| | 20 | Amana Maalumu | 173,279 | 172,011 |
| | 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 16,114 | 7,206 |
| | 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0 | -0 |
| | 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 18,769 | 18,850 |
| | 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| | 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| | 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa | 2,726 | 2,547 |
| | 27 | Dhima Nyingine | 35,252 | 32,028 |
| | 28 | Madeni | 98,641 | 100,429 |
| | **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,254,871** | **1,203,989** |
| | **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI *(16 kutoa 29)*** | **133,159** | **123,338** |
| C. | | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,372 | 31,372 |
| | 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| | 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 75,076 | 74,499 |
| | 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 15,144 | 7,773 |
| | 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 11,567 | 9,694 |
| | 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| | **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **133,159** | **123,338** |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-23 | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30/09/2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-23 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-22 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 41,803 | 34,319 | 113,068 | 103,672 |
| 2 Gharama za Riba | (12,322) | (12,988) | (38,313) | (35,563) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **29,481** | **21,331** | **74,755** | **68,109** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 73 | (548) | (92) | (604) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (2,913) | (3,435) | (8,420) | (10,349) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **9,484** | **10,632** | **30,641** | **26,846** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za | (370) | 1,344 | 4,164 | 3,965 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 7,244 | 4,903 | 17,545 | 13,774 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 2,610 | 4,384 | 8,932 | 9,107 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(27,015)** | **(24,500)** | **(76,983)** | **(73,312)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 12,855 | 11,804 | 37,933 | 36,296 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 2,822 | 2,125 | 6,930 | 5,497 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 11,338 | 10,572 | 32,120 | 31,518 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **9,110** | **3,479** | **19,901** | **10,691** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 1,737 | 1,521 | 4,759 | 5,014 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **7,373** | **1,958** | **15,144** | **5,677** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **7,373** | **1,958** | **15,144** | **5,677** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 1,081 | 1,089 | 1,081 | 1,089 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 1,931 | 62 | 1,931 | 181 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 52 | 48 | 52 | 48 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.50% | 0.15% | 1.10% | 0.46% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 5.60% | 1.66% | 12.00% | 4.88% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 53.00% | 54.51% | 54.00% | 56.17% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3.00% | 2.04% | 7.00% | 6.74% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA SEPTEMBA, 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Robo Mwaka va sasa 30-Sep-23 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-23 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-23 | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-22 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 9,110 | 7,118 | 19,901 | 10,691 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 5,433 | 5,943 | 16,596 | 18,814 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (61,733) | 9,678 | (57,304) | (103,278) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 0 | 0 | 0 | 0 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 40,441 | 10,446 | 96,199 | 74,187 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | 0 | 0 | 0 | 0 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 3,143 | 1,014 | 41,588 | 4,648 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (5,407) | 1,425 | 71,149 | (4,997) |
| - Kodi Iliyolipwa | (1,737) | (1,737) | (4,759) | (5,014) |
| - Mengineyo (bainisha) | 56,416 | (8,956) | (42,862) | (47,956) |
| ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **45,666** | **24,931** | **140,508** | **(52,906)** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (698) | (1,308) | (2,616) | (2,193) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo (fedha iliyotolewa na serikali) | 0 | (30,000) | 0 | 0 |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(698)** | **(31,308)** | **(2,616)** | **(2,193)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | (1,652) | (999) | (4,035) | (5,164) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | ***(1,652)*** | ***(999)*** | ***(4,035)*** | ***(5,164)*** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 43,317 | (7,376) | 133,857 | (60,263) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **115,751** | **123,127** | 25,211 | **157,687** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 159,068 | 115,751 | 159,068 | 97,424 |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2023

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **31,372** | - | **75,565** | - | **0** | **9,694** | **116,632** |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | | | | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | - | - | - | | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 15,144 | - | - | - | **15,142** |
| Mapato mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | | | - | - | | | |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo(Fedha iliyotolewa na serikali) | - | - | **1,384** | - | | - | **1,384** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,372** | - | **92,091** | - | **0** | **9,694** | **133,158** |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **74,709** | **739** | **0** | **9,694** | **113,214** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka 2022 | - | - | 3,154 | - | - | - | **3,154** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | 630 | - | - | - | **630** |
| Hisa za ziada(Issued bonus shares) | **3,300** | - | **(3,300)** | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | **739** | **(739)** | - | - | - |
| Kodi iliyolipwa kwenye share za bonasi | - | | **(367)** | | | | **(367)** |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yaliyofafanuliwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Kurudishiwa Gawio lililosimamishwa | | | - | | | | - |
| Mengeineyo | - | | - | | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,372** | - | **75,565** | - | **0** | **9,694** | **116,631** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA, 2023

Benki ililipa faini ya shilingi 62,000.00 kutokana na upungufu wa fedha zilizopelekwa Benki kuu (Bot Counter shortage)
Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| **SABASABA K. MOSHINGI** (Ofisa Mtendaji Mkuu) | Imesainiwa | **25.10.2023** |
| **REGINA E. SEMAKAFU** (Mkurugenzi wa Fedha) | Imesainiwa | **25.10.2023** |
| **SOSTHENES F. NYENYEMBE** (Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani) | Imesainiwa | **25.10.2023** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA** Mwenyekiti wa Bodi | Imesainiwa | **25.10.2023** |
| **MR. GILBERT W. CHAWE** Mjumbe wa Bodi | Imesainiwa | **25.10.2023** |

tcbbank

Head Office, Millenium Tower II, 10th Floor, Kijitonyama Opp. Makumbusho Village,
P.O. Box 9300, Dar Es Salaam | Telephone; +255 22 216 2940
E-mail: info@tcbbank.co.tz | www.tcbbank.co.tz | Customer Care: +255 787 669977 | +255 788 767 683 | +255 658 767 683

TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

# MINIMUM DISCLOSURE OF RATES AND CHARGES 2023

*All charges are VAT exclusive.

| PRODUCT | MINIMUM OPENING BALANCE | | | | MONTHLY MAINTANCE FEES | | | | MINIMUM OPERATING BALANCE | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS | USD | EUR | GBP | TZS | USD | EUR | GBP | TZS | USD | EUR | GBP |
| Call account | 100,000.00 | 100.00 | N/A | 100.00 | 10,000.00 | 5.00 | N/A | 100.00 | 100,000.00 | 100.00 | N/A | 100.00 |
| Business Current Account | 100,000.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 | 20,000.00 | 20.00 | 100.00 | 100.00 | 100,000.00 | 100.00 | 100.00 | 100.00 |
| Personal current Account | 100,000.00 | 100.00 | N/A | N/A | 7,000.00 | 5.00 | N/A | N/A | 50,000.00 | 100.00 | N/A | N/A |
| Vikundi Current Account | 100,000.00 | N/A | N/A | N/A | FREE | N/A | N/A | N/A | 50,000.00 | N/A | N/A | N/A |
| Quick Account | 20,000.00 | 10.00 | N/A | 10.00 | 1,800.00 | 0.86 | N/A | 10.00 | 20,000.00 | 10.00 | N/A | 10.00 |
| Salary Account | FREE | N/A | N/A | N/A | 1,800.00 | N/A | N/A | N/A | 0 | N/A | N/A | N/A |
| Tabasamu Individual | 10,000.00 | N/A | N/A | N/A | FREE | N/A | N/A | N/A | 10,000.00 | N/A | N/A | N/A |
| Tabasamu Group Account | 50,000.00 | N/A | N/A | N/A | FREE | FREE | N/A | N/A | 50,000.00 | N/A | N/A | N/A |
| Platinum Account | FREE | N/A | N/A | N/A | FREE | N/A | N/A | N/A | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| Minor Account | 20,000.00 | N/A | N/A | N/A | FREE | N/A | N/A | N/A | 20,000 | N/A | N/A | N/A |
| Group Account | FREE | N/A | N/A | N/A | FREE | N/A | N/A | N/A | 0 | N/A | N/A | N/A |
| Scout Minor Account | 10,000.00 | N/A | N/A | N/A | FREE | N/A | N/A | N/A | 10,000 | N/A | N/A | N/A |
| Scout Account | 30,000.00 | N/A | N/A | N/A | FREE | N/A | N/A | N/A | 30,000 | N/A | N/A | N/A |
| Wavuvi Account | 10,000.00 | N/A | N/A | N/A | 1,800.00 | N/A | N/A | N/A | 10,000 | N/A | N/A | N/A |
| Wadu Account | FREE | N/A | N/A | N/A | FREE | FREE | N/A | N/A | 10,000 | N/A | N/A | N/A |
| Kivulini Account | FREE | N/A | N/A | N/A | 700.00 | N/A | N/A | N/A | 1,500.00 | N/A | N/A | N/A |

## CASH SERVICES

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Cash deposit | | FREE |
| Cash withdrawal TZS | 0 - 100,000 | 3,000 |
| | 100,001 - 400,000 | 3,000 |
| | 400,001 - 500,000 | 4,400 |
| | 500,001 - 800,000 | 4,400 |
| | 800,001 - 1,000,000 | 5,200 |
| | 1000,001- 1,200,000 | 5,200 |
| | 1000,001 - 2,000,000 | 6,100 |
| | 2000,001 - 3,000,000 | 6,100 |
| | 3000,001 - 5,000,000 | 6,100 |
| | 5000,001 - 10,000,000 | 0.12% - 170,000 |
| | 1000,0001 - 15,000,000 | 0.12% - 170,000 |
| | 1500,0001 - 25,000,000 | 0.12% - 170,000 |
| | 25,000,000 - 50,000,000 | 0.12% - 170,000 |
| | 50,000,000 - 100,000,000 | 0.12% - 170,000 |
| | 100,000,001 - Above | 0.12% - 170,000 |
| Cash withdrawal USD | Withdrawal below 50 | 1.00 |
| | Withdrawal from 51-1,000 | 2.50 |
| | Withdrawal from 1,000 -2,250 | 5.00 |
| | Withdrawal from 2,251-5,000 | 15.00 |
| | Withdrawal Above 5,000 | 0.25% |
| **BANK STATEMENT** | **TZS** | **USD** |
| Balance enquiry over the counter | 2000.00 | USD equivalent |
| Statement per page | 2,000.00 | USD equivalent |
| **CHEQUE SERVICE** | **TZS** | **USD** |
| Cheque book per leaf | 500.00 | USD equivalent |
| Cheque clearing | FREE | FREE |
| Unpaid cheque/insufficient fund | 150,000.00 | USD equivalent |
| Stop Payment order | 30,000.00per leaf Max 300,000.00 | USD equivalent |

## AGENT BANKING SERVICE

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Deposit | PER TRANSACTION | FREE |
| Withdrawal | 0.01 - 10,000.00 | 800.00 |
| | 10,000.01 - 20,000.00 | 1,250.00 |
| | 20,000.01 - 50,000.00 | 1,500.00 |
| | 50,000.01 - 100,000.00 | 2,250.00 |
| | 100,000.01 - 200,000.00 | 2,750.00 |
| | 200,000.01 - 300,000.00 | 4,200.00 |
| | 300,000.01 - 400,000.00 | 5,500.00 |
| | 400,000.01 - 500,000.00 | 6,000.00 |
| | 500,000.01 - 700,000.00 | 6,500.00 |
| | 700,000.01 - 1,000,000.00 | 7,500.00 |
| | 1,000,000.01 - 1,500,000.00 | 8,500.00 |
| | 1,500,000.01 - 2,000,000.00 | 9,000.00 |
| | 2,000,000.01 - 5,000, 000.00 | 10,000.00 |
| | 5,000,000.01 - 6,000,000.00 | 11,000.00 |
| | 6,000,000.00 - 7,000,000.00 | 12,000.00 |
| | 7,000,000.00 - 8,000,000.00 | 13,000.00 |
| | 8,000,000.00 - 9,000,000.00 | 14,000.00 |
| | 9,000,000.00 - 10,000,000.00 | 15,000.00 |
| Balance Enquiry | | 300.00 |
| Mini Statement | | 300.00 |

## POPOTE MOBILE BANKING / INTERNET BANKING

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Registration | | FREE |
| Transfer Bank to MNO | 0-9,999.99 | 1,100.00 |
| | 10,000 - 19,999.99 | 2,000.00 |
| | 20,000 - 29,99.99 | 2,500.00 |
| | 30,000 - 39,999.99 | 3,200.00 |
| | 40,000 - 49,999.99 | 3,400.00 |
| | 50,000 - 99,999.99 | 4,100.00 |
| | 100,000 - 199,999.99 | 4,800.00 |
| | 200,000 - 249,999.99 | 5,500.00 |
| | 250,000 - 299,999.99 | 6,000.00 |
| | 300,000 - 399,999.99 | 6,500.00 |
| | 400,000 - 699,999.99 | 7,100.00 |
| | 800,000 - 999,999 | 9,500.00 |
| | 1000,000 - 1,999,999 | 11,000.00 |
| | 2000,000 - Above | 12,500.0 |
| From MNO to Bank (Deposit) | | FREE |

## LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES

| LOANS | CATEGORY | RATE |
|---|---|---|
| Consumer loans | Consumer loan Admnistartion fee | 1.5% of the Approved Loan Minimum TZS 20,000.00 |
| Wastaafu Loans | Loan Application fee | TZS 20,000.00 |
| | Loan Administration fee | 1.5% Minimum TZS 20,000.00 Maximum TZS 150,000.00 |
| Other Charges On individual Micro Credit | MIC loan Application fee | TZS 150,000.00 |
| | MIC loan processing/Administration fee | 1.5% Minimum TZS 150,000.00 |
| Charges on Business Loan | Loan Applicationfee for Business Loans | TZS 200,000.00 |
| | Loan Administration fee- Business and Personal loans | 2% of the Approved Amount |

| DORMANT ACCOUNT | | |
|---|---|---|
| Dormant account fee | FREE | |
| Re-activation | FREE | |

| ACCOUNT CLOSURE | TZS | USD |
|---|---|---|
| Closing account fee | 13,000.00 | USD equivalent |

| OTHER SERVICES | TZS | USD |
|---|---|---|
| Government Securities transaction Handling fees | 50,000.00 | N/A |
| Confirmation to Auditors | 45,000.00 | USD equivalent |
| Introduction letter/Confirmation to Embassies | 45,000.00 | USD equivalent |

| FUND TRANSFER SERVICE | TZS | USD |
|---|---|---|
| TISS-Outward | 10,000.00 | USD Equivalent |
| TISS-Inward | FREE | FREE |
| EFT-Outward | 2,000.00 | N/A |
| EFT-Inhouse | 1,500.00 | N/A |
| TT-Outward | N/A | 55 |
| TT-Inward | N/A | 5 |
| Internal Transfer | FREE | FREE |
| Standing Order - Within the Bank | FREE | FREE |
| Standing Order - To other Bank | 13,000.00 | USD Equivalent |
| Salary Handling-Cheque list | 1,000.00 | USD Equivalent |

## POPOTE ATM SERVICE

| ACTIVITY | BAND [TZS] | New Charge (TZS) |
|---|---|---|
| 1. ATM Cash Withdraw | 1,000 – 99,000 | 1,500 |
| | 100,000 – 400,000 | 1,700 |
| 2. Interbank transfer on ATM | 1 – 99,999 | 1,300 |
| | 100,000 - 199,999 | 1,700 |
| | 200,000 - 299,999 | 1,700 |
| | 300,000 - 399,999 | 1,700 |
| | 400,000 - 499,999 | 2,500 |
| | 500,000 - 599,999 | 3,000 |
| | 600,000 - 699,999 | 3,500 |
| | 700,000 - 999,999 | 4,000 |
| | 1,000,000 - 1,999,999 | 5,000 |
| | 2,000,000 - 2,999,999 | 6,000 |
| | 3,000,000 - 3,999,999 | 7,000 |
| | 4,000,000 - 4,000,000 | 8,000 |
| 3. Intra-Bank Transfer on ATM | Any Amount | 1,000 |
| 4. Balance Inquiry | NA | 400 |
| 5. Mini Statement | NA | 400 |
| 6. Popote ATM card issuance /Replacement | N/A | 15,000 |
| 7. Annual Card maintainance | N/A | 10,000 |
| 8. PIN Re-issue | N/A | 1,000 |
| 9. Collection of ATM card at non-domicileBranch | N/A | 6,500 |
| 10. Uncollected and Destroyed ATM Card | N/A | N/A |
| 11. Failed Transaction Due to insufficient fund | | 900 |

| LETTER OF CREDIT ISSUED (IMPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Charges on Draft LC | USD 60 |
| LC commission per quarter | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| LC commission per quarter with cash cover | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1% perquarter Min USD 150 or foreign eqv |
| Other amendments | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Discrepancy fee per pack | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Documen examination Fee per pack | 0 |
| Cancellation charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Non-Payment of Bills Due Date | 0 |
| Expire unutlised Letters of Credit | 0 |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Advising Fee or commission | USD 200 or foreign eqv |
| Bank client for LC available with us | USD 150 or foreign eqv |
| Client for LC available with other Bnaks | N/A |
| Non Bank Customer | USD 250 or foreign eqv |
| Confirmation Fee(per quarter)USD eqv | 1% per quarter and part thereof,Min USD 250 or foreign eqv |
| Amendment advising Fee | USD 120 or foreign eqv |
| Cancellation Fee | USD 60 or foreign eqv |
| Transfer Fee (per quarter) | 0.75% per quarter, Min USD 250 or foreign eqv |
| Courier services | Actual costs plus USD 10 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv |
| Document Handling commission | N/A |
| Discrepancy Fee per document | N/A |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Commission on LC discounting/Negotiation | 0.75% Min USD 200 Max 600 or foreign eqv |
| Negotiation Bills under an Export Letter of Credit (Discounting Bills) | N/A |
| Extension - Commission for unconfirmed LC | 0.5% per quarter and part thereof, Min of USD 200 or foreign eqv |
| Extension - Commission for confirmed LC | 1% per quarter and part thereof Min. of USD 100 or foreign eqv |


| COLLECTION (DOCUMENTARY CREDIT) | CHARGES |
|---|---|
| Documents processing | 1% Min USD 15 Max 200 |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 |
| **Outward Documentary bills for collection (OFBC)** | |
| Document handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 350 or foreign eqv |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 or foreign eqv |
| Chaser/Tracer | USD 60 or foreign eqv. |
| **Inward Documentary bills for collection** | |
| Bill discounted handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 600 or foreign eqv |
| Document returned unpaid or unaccepted | 0 |
| For each amendment of previous instructions | 0 |
| Every presentation or reminder protest fee | 0 |
| Delivery of documents for non - customers | USD 250 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Payment commission for documents value greater than USD 50,000 | 0 |
| Payment commission for documents value less than USD 50,000 | 0 |
| Avalisation commission per quarter or part thereof | 1.20% |
| Risk margin on acceptance (per quarter) | 1.20% |

## GUARANTEE

| | CHARGES |
|---|---|
| Issuance or confirmation of foreign Currency guarantee Commission(per quarter) | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Bid bond | 1.0% Bid bond Issuance part thereof Min TZS 150,000 of USD 64 foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Perfomance,Advance Payment and any other bank guarantees | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 350,000 or USD 150, foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Text amendment fee | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |
| Other amendments | USD 60 or foreign eqv |
| Guarantee advisisng fee (from other Banks) | USD 200 or foreign eqv |
| Courier services (Direct delivery to Beneficiary) | 0 |
| Open ended guarantees(charged per annum) | 3%p.a |
| Cancellation | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |

## POPOTE VISA CARD

| DESCRIPTION | CHARGES |
|---|---|
| Popote VISA issuance/Replacement | 15,000.00 |
| Annual Card Maintainance | 10,000.00 |
| ATM Withdrawal - Domestic | 3,500.00 |
| Balance Inquiry - Domestic | 1,000.00 |
| ATM Withdrawal - International | 6,000.00 |
| Balance Inquiry - International | 2,000.00 |




Makao Makuu, PSSSF, Millenium Towers II, Barabara ya Bagamoyo, S.L.P. 9300, Dar es Salaam, Tanzania. Simu +255 22 2162940, Faksi +255 22 2114814

Huduma kwa Wateja: +255 22 787 669977, +255 788767683, +255 658 767683
Namba bila Malipo: 0800110160

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania wajifunze kujikinga magonjwa yanayoweza kuzuilika

**MARADHI** ya vidonda vya tumbo ni miongoni mwa magonjwa ambayo yanaathiri moja kwa moja mfumo wa chakula, huku watu wazima wakiwa katika hatari hiyo zaidi.

Kumekuwa na ongezeko la wanaougua maradhi hayo, ambao kwa simulizi zao wanabainisha namna wanavyoishi na shida hiyo, wakilazimika kutumia dawa kila siku kukabiliana na kiwango kikubwa cha 'acid' (tindikali) inayozalishwa tumboni.

Bingwa wa Upasuaji na Mkuu wa Idara ya Upasuji Hospitali ya Taifa Muhimbili- Mloganzila, Dk. Eric Muhumba hivi karibuni katika mazungumzo na Nipashe, ametoa wito kwa jamii kuhusu ugonjwa huo.

Anasema mfumo wa chakula ni sehemu zote za mwili chakula kinapopita, kuanzia mdomoni hadi sehemu ya kutoa haja, hivyo mfumo huo, ndio uhai wa binadamu kwa kuwa kila kiungo mwilini kinategemea chakula kutoka kwenye mfumo huo.

Ameeleza, wengi wanaougua huwa katika mfumo wa ulaji chakula wenye masharti, sababu kuu ni kuepuka maumivu yatokanayo na mlo watakaoutumia iwapo unaathiri mfumo wa chakula.

Tatizo lingine linalosababisha ni msongo wa mawazo, utokanao na changamoto za maisha kuwa ni kati ya sababu za ugonjwa huo, lakini hata ulaji wa chakula kilichoandaliwa katika mazingira machafu.

Watu wengi hivi sasa wanapenda kuweka miili yao katika umbile la kawaida na kujinyima chakula, Bingwa huyo anasema, pia kukaa muda mrefu bila mlo, ni sababu nyingine za maradhi hayo, akisema katika hospitali hiyo hupokewa wagonjwa wawili hadi watano kwa siku.

Tahadhari inayotolewa na daktari huyo kwa jamii ni kwamba wasijenge tabia ya kukaa muda mrefu bila kula na wanaougua kuepukana na ulaji wa vyakula vyenye 'acid' zaidi.

Vyakula hivyo kuwa ni kama vile maziwa, maharage, vyakula vyenye viungo vingi, akisema vinachangia kumuongezea maumivu anayeugua.

Baadhi ya watu wanaougua ugonjwa huo hufikiri maziwa yanatuliza maumivu, lakini kumbe wanajiongezea tatizo.

Daktari anasema kuna athari kubwa itokanayo na vidonda vya tumbo kama vile kuta za tumbo kuvimba na kuziba njia ya chakula kuingia kwenye utumbo mdogo, jambo ambalo linaloweza kuhitaji upasuaji wa haraka.

Pamoja na kwamba kumekuwa na hali tofauti za kiuchumi kwenye jamii, hasa kupatikana kwa mlo kamili wa siku, jamii inaweza kuwa na mbinu tofauti, ili kukabiliana na hali hiyo.


Kwa maana kwamba jamii inaweza kujipatia au kununua chakula maeneo ya sokoni, magengeni, ambako huuzwa kwa gharama nafuu ikiwamo matunda na kukiandaa kwa kupika au kula, ili kupunguza athari, ambazo zitasababishwa na tumbo kuwa tupu kwa saa nyingi.

Upo usemi kwamba kinga ni bora kuliko tiba. Kula chakula kwa kuzingatia muda ni nafuu kuliko kutumia gharama kubwa za matibabu ambazo zingeweza kuepukika.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo, matibabu ya maradhi hayo yana ugumu kwa sababu 'acid' inazalishwa na mwili na wakati huo huo tiba kubwa ni kupunguza uzalishaji wa 'acids'.

Wito kwa jamii ni kujenga tabia ya kutenga muda wa kupata hata mlo wa kawaida kama vile matunda, kwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizojaliwa vyakula vya aina tofauti na bei nafuu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Hili la bodaboda kufanya wanavyotaka, halikubaliki

Na Mary Seme

**IMEKUWA** ni kawaida kwa madereva wa pikipiki za abiria 'bodaboda' kuvunja kanuni za usalama barabarani jambo ambalo si sawa. Umekuwa ni kama utaratibu wa kawaida kiasi kwamba hata polisi wa usalama barabarani siku hizi hawatilii mkazo kuwafuatilia madereva hao na hivyo kuhalalisha uvunjifu wa sheria za usalama barabarani.

Imefikia wakati ukitaka kuvuka barabara kutoka upande mmoja kwenda upande wa pili unakuwa makini zaidi na madereva wa bodaboda kuliko wa magari kwa jinsi wanavyoendesha kwa fujo boda boda zao na usipokuwa muangalifu unagongwa .Sina hakika kama madereva hawa wote wana elimu ya kutosha kuhusu usalama barabarani kama inavyotakiwa.

Kipindi fulani bunge liliwaka moto kutokana na mjadala uliokuwapo wa kutaka faini ya bodaboda kupunguzwa hadi shilingi 10,000 ambapo kwa wakati huo ilikuwa ni shilingi 30,000 ambayo baadhi ya wadau wakiwemo wabunge walidai kiwango kilichokuwepo kilikuwa kikiwaumiza madereva hao na mwisho kuamuliwa kwamba kipunguzwe.

Baadhi ya waliokuwa wakipinga kupunguzwa kwa faini hiyo walijenga hoja ya kwamba madereva hao ni wasumbufu na hivyo kuwapunguzia kiwango cha faini kungeongeza kiwango cha usumbufu wao barabarani na hivyo kuchochea zaidi uvunjifu wa sheria za usalama barabarani jambo ambalo linaonekana kwa sasa.

Ni muhimu sasa ukatafutwa ufumbuzi wa tatizo hili kabla taifa halijajaa vilema na kupungukiwa kwa nguvu kazi kutokana na ajali za bodaboda tunazoshuhudia barabarani , hasa kwa kuzingatia kuwa bodaboda imekuwa ajira kwa vijana wengi waliokosa ajira rasmi katika ofisi za serikali na watu binafsi na hivyo bodaboda ndiyo kimbilio lao.

**Madereva wa magari wanakuwa makini kwa kuogopa kulipa faini ya shilingi 30,000 ni mara chache kukuta wamevuka barabara bila taa kuwaruhusu au wamepita njia isiyowahusu lakini jambo kama hilo ni la kawaida kwa madereva wa bodaboda utakuta wa magari wamesimama lakini wao wanakatisha bila kuruhusiwa na taa za kijani.**

Polisi Idara ya Usalama Barabarani isilifumbie macho tatizo hili kwa sababu tu ya faini kidogo wanayotakiwa kutoa madereva wa bodaboda pindi wanapokamatwa kwa kuvunja sheria za usalama barabarani na kukimbilia kuwakamata madereva wa magari pekee ambao pengine ni kwa sababu faini yake ni kubwa.

Madereva wa magari wanakuwa makini kwa kuogopa kulipa faini ya shilingi 30,000 ni mara chache kukuta wamevuka barabara bila taa kuwaruhusu au wamepita njia isiyowahusu lakini jambo kama hilo ni la kawaida kwa madereva wa bodaboda utakuta wa magari wamesimama lakini wao wanakatisha bila kuruhusiwa na taa za kijani.

Ni kana kwamba wao huwa wana haraka kuliko madereva wa vyombo vingine ,pia utakuwakuta wakikatisha njia ya wapita kwa miguu na kuwaletea usumbufu waendao kwa miguu bila kuthibitiwa na mtu yeyote, mbaya zaidi huwa ni wakali sana pale mmoja wao anapothibitiwa na wananchi kutokana na kuvunja sheria za usalama barabarani kiasi kwambo wapo tayari kuanzisha vurugu katika harakati za kumetetea mwenzao huyo.

Ifike mahali kama si kurejeshwa kwa faini ya shilingi 30,000 kwa madereva wa boda boda basi pawepo na darasa maalum katika idara ya polisi kitengo cha usalama barabarani hasa katika miji mikubwa ili kuthibiti wimbi hili la uvunjifu wa sheria za usalama barabarani.

Kipindi fulani aliyewahi kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola alitaka kuweka mkakati wa kila pikipiki kufungwa tela ili kutokuwapa urahisi wa kupenya kirahisi tu kila mahali ingawa alipingwa vikali lakini inaonyesha jinsi tatizo lilivyo.

KESI MAUAJI DADA BILIONEA MSUYA

# Mke wa Bilionea Msuya: Nilipelekwa porini, wakanihoji wakiwa na bastola

**Na Grace Gurisha**

MIRIAM Mrita, aliyekuwa mke wa mfanyabiashara wa madini mkoani Arusha, Erasto Msuya 'Bilionea Msuya', amedai Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Arusha, SSP David Mhanaya, akiwa na wenzake wawili, walimpeleka porini, wakamhoji dai lao la kumuua Aneth wakiwa na bastola.

Pia amedai hakuna shahidi yeyote wa upande wa mashtaka aliyewasilisha ushahidi wa kuonesha ujumbe ambao alikuwa wakijibizana na marehemu wifi yake, Aneth Msuya (pichani chini).

Miriam ambaye anatuhumiwa kuhusika na kifo cha wifi yake Aneth cha Mei 25, 2016, alidai hayo jana mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam wakati akiendelea kutoa utetezi wake.

Alidai kuwa kuhusu ujumbe wa simu kati yake na marehemu Aneth, haujathibitishwa na shahidi yeyote. Pia hadi sasa simu zake zilichukuliwa na askari polisi waliomkamata.

"Simu wanazo wao askari na kulikuwa na wapelelezi na kama kulikuwa na ukweli wa kutumiana meseji, mashahidi wa upande wa mashtaka wangeuleta maana simu zangu wanazo na simu za Aneth wanazo. Kwahiyo, ushahidi wao ni wa uongo," alidai.

Akiendelea kuongozwa na Wakili wake, Peter Kibatala, Miriam alidai hoja ya SSP Mhanaya kwamba alipanga njama ya kumuua Aneth kwa sababu ya mirathi si ya kweli. Aliwagawia mali ndugu wa marehemu kwa kuwa ana upendo.

Alidai kuwa Jaji Kamuzora katika uamuzi aliousikiliza kwa njia ya video, alisema kwamba yeye hastahili kuwa msimamizi kwa sababu hakupeleka mrejesho wa ukusanyaji mali kwa wakati, pia kwa sababu yuko gerezani, hawezi kufanya majukumu mengine.

Pia alidai kuwa hakuna mahali Jaji Kamuzora wa Mahakama Kuu Arusha alisema anamtoa yeye na kuweka watoto wake kwa sababu nyingine yoyote ile.

Miriam alidai kuwa sababu ya mama mkwe wake, Ndeshukurwa kupeleka maombi mahakamani ili yeye atolewe ni kushindwa kutoa mrejesho. Ilikuwa mwaka 2019 akiwa katika Gereza la Segerea.

Alidai kuwa, asubuhi ya Agosti 9, 2016 SSP Mhanaya, Afande Malangahe na Latifa, saa tisa walinitoa nje wakampeleka kwenye gari akiwa amefungwa macho na baada ya kutembea umbali fulani afande Latifa akamfungua kitambaa.

"Nilijikuta nipo katikati ya pori wakawa wananihoji kwa nini nilimuua Aneth na wote; Mhanaya, Malangahe na Latifa walikuwa na bastola na Mhanaya alikuwa ananigongagonga kichwani na kitako cha bastola," alidai.

Miriam alidai kuwa alimwuliza kama anapafahamu mahali hapo, akajibu kwamba hapafahamu, akamwambia hata wakimuua, hakuna ndugu yake yeyote angefahamu.

"Walinipiga sana, baadaye nikafungwa tena kitambaa usoni wakanirudisha kwenye gari, safari ikaanza nikafunguliwa kitambaa nikiwa tena Kituo cha Polisi Airport, ambako walinishusha wakaniingiza tena mahabusu," alidai.

Alidai kuwa Agosti 10, 2016, Mhanaya, Malangahe na Latifa Chiko walimfuata mchana, akaingia nao kwenye chumba kingine, akaja kijana mwingine ambaye ni Kasigwa, shahidi wa sita wa upande wa mashtaka.

"Kulikuwa na kiti nikawekewa fimbo shingoni nikainuliwa miguu na Kasigwa akawa ananipiga chini ya miguu, wananiuliza kwanini nimemuua Aneth, lakini nikasema sijamuua," alidai.

Aliendelea kudai kuwa baadaye walimrudisha mahabusu na Agosti 11, 2016 mchana, wakaenda tena wakamchukua kwenye gari wakiwa na vijana wengine, akafungwa kitambaa usoni.

"Baada ya umbali fulani walisimama, nikashushwa kwenye gari nikasogezwa mbele kidogo, nikafunguliwa kitambaa, wakaanza kunipiga tena na Mhanaya akauliza kama kuna chupa kwenye gari niingiziwe kwenye makalio na Latifa akasema au achomwe na bisibisi sehemu za siri ili nikiri kwamba nimemuua Aneth.

"Baada ya kunipiga sana nikapandishwa tena kwenye gari, tukatoka kwenye hilo pori hadi maeneo ya Chalinze na muda huo ilikuwa ni usiku na baadaye wakanirudisha Airport na nyakati zote hizo nilipokuwa ninarudishwa nilikuwa ninashinda na Arafa," alidai.

Aliendelea kudai kuna siri inaendelea kwa kuwa anaamini haiwezekani dada wa kazi wa marehemu Aneth Msuya, Getruda Mfuru apatikane baada ya miezi miwili ya tukio hilo la mauaji kutokea.

Alidai kuwa Jeshi la Polisi lina mtandao mkubwa wa mawasiliano na wapelelezi wengi, hivyo haiwezekani washindwa kumpata dada wa kazi kwa sababu katika ushahidi wa RCO Richard Mchovu alidai kuwa mama wa marehemu ndiye aliyempa taarifa kuwa dada huyo yuko Masama, Moshi.

"Dada huyo alikiri mbele ya mahakama kwamba hakuwahi kubadilisha namba yake ya simu na muda wote ilikuwa hewani na pia huyo mama wa marehemu hakuwahi kuja kutoa ushahidi hapa mahakamani kueleza jambo kubwa hilo alilolifanya," alidai.



Miriam pia alidai anashangaa upande wa mashtaka kushindwa kumleta mahakamani mpenzi wa Getruda Mfuru, Sabri Kombo ili aeleze kwamba yeye ndiye aliyempa nauli ya kurudi kwao Masama, Moshi.

Kesi inaendelea kusikilizwa leo kwa upande wa utetezi kumhoji shahidi huyo.

# DART yapata mwarobaini kero mabasi mwendokasi

**Na Joseph Mwendole**

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART) umepata mkandarasi mshauri wa kubuni mfumo wa kisasa wa kuongoza mabasi katika njia zake.

Mkandarasi huyo kampuni ya IDOM ya Hispania itabuni mfumo huo uitwao Intelligent Transportation System (ITS) ndani ya miezi mitano na tayari ameshaanza kufanya kazi hiyo. Akizungumza katika mkutano wa wadau kuhusu mfumo huo, Mtendaji Mkuu wa DART, Dk. Edwin Mhede, alisema jana kuwa kuanzishwa kwa mfumo huo kunaonesha dhamira ya dhati ya serikali kuboresha usafiri wa umma.

Alisema mfumo huo mpya utakuwa na manufaa makubwa kwa kuwa mbali na kuwapa huduma bora wasafiri wanaotumia usafiri huo pia utawahakikishia usalama wao. Alisema kwa mujibu wa makubaliano na mkandarasi huyo mshauri, mfumo huo unatakiwa uanze kufanya kazi kabla ya mwezi Juni mwakani.

Dk. Mhede alisema wamekubaliana na mkandarasi huyo mshauri kuwa kutakuwa na programu za kuwajenga uwezo wataalamu wa ndani ili wamudu kuuendesha baada ya kuusimika.

Meneja Mipango wa Usafiri wa DART, Mohamed Kuganda, alisema kampuni ya IDOM ya Hispania itabuni mfumo huo wa ITS na baada ya kukamilisha itatangaza zabuni ya kumpata mkandarasi atakayefunga vifaa vilivyobuniwa ndani ya mfumo huo. Alisema, mfumo huo wa kisasa utasaidia kwa kiasi kikubwa kuongoza magari na kutoa taarifa mbalimbali ambazo ni muhimu kwa abiria wanaotumia usafiri wa mabasi hayo.

"Ukiona mtu amekaa kwenye kituo cha basi kuna maelekezo anayapata kwamba basi linalofuata litaondoka muda flani hizo taarifa zinatokana na mfumo huu wa ITS," alisema.

Alisema ndani ya mfumo huo wa ITS kutakuwa na mfumo mwingine utakaoziwezesha taa za barabarani kuwaka kijani kila mabasi hayo yatakayokuwa yakipita ili yawahishe abiria.

"Hii inaitwa Public Transport Priority Signal, basi likifika tu taa zitajibadilisha haraka zinakuwa za kijani na basi litapita bila kusubiri kama ilivyo kwa sasa na utatuwezesha kuyapanga vizuri haya mabasi tofauti na ilivyo sasa.

"Kwa mfumo huu maisha ya wanayotumia mabasi yaendayo haraka yatakuwa rahisi sana kwa sababu mtu atafika kwenye kituo ataona basi linalofuata linafika baada ya dakika ngapi. Kwahiyo, hakutakuwa na haja ya kugombania kwa sababu ratiba nzima itaonekana pale na kama basi limejaa anasubiri linalofuata," alisema Kuganda.

**FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED** Housing

**FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED** commenced its operations in October 2017 as a fully-fledged financial institution specializing on the provision of residential mortgages. The company was licensed by Bank of Tanzania in July 2017 to commence housing finance business under the provisions of The Banking and Financial Institutions Act, 2006 (Cap. 342. R.E. 2002).

**FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED** is seeking to recruit competent direct sales officers who have hands-on skills in marketing and selling mortgage products and services to support growth of our mortgage portfolio, if you are enthusiastic about sales and you are excellent at prospecting customers, good communication skills, social selling and excellent negotiation skills and presentation skills, feel free to apply on this challenging posts for further growing and sharpening your career.

| | | |
|---|---|---|
| Job Title | : | Direct Sales Agencies (3 positions) |
| Reporting to | : | Business Manager |
| Location | : | Dar Es Salaam |

**Job Description**
- Promotes and sells various mortgage products offered by the company, aiming to attract low cost mortgages from diverse customer segments.
- Prospects for new customers through existing leads, referrals, calling etc. and maximizing lead generation.
- Ensures timely follow through and healthy closure rate of leads.
- Achieves ascribed monthly sales target.
- Informs customers of new products or product enhancements to further expand the banking relationship and enhance customer value.
- Establishes and maintains effective relationships with customers, and maintains high level of customer service.
- Advises customers on available bank products and services based on understanding of customers' financial needs and recommends appropriate solutions.
- Cross-sells secured assets offered.
- Adheres to expected level of due-diligence, internal policies and KYC norms and AML policy norms.

**Qualifications and Competencies**
- Education-At least Diploma in Marketing, Banking and Finance, Economics or related field
- Business and Sales Acumen
- Negotiation Skills
- Organizing and Planning
- Good communication and Presentation skills
- Emotional awareness
- Relationship Building and Management

**Applications: Qualified candidates to Send CV and application letter to: info@firsthousing.co.tz**

**Deadline: 03rd November 2023.**

217672101

# BENKI YA STANBIC TANZANIA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa | Robo Mwaka/Mwaka uliopita |
|---|---|---|---|
| | | 30-Sep-23 | 30-Jun-23 |
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 23,244 | 28,758 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 217,783 | 221,163 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 412,717 | 376,553 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 64,774 | 135,075 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 83,925 | 69,884 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 506,914 | 351,343 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 1,218,903 | 1,244,236 |
| 12 | Mali Nyingine | 72,550 | 75,465 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 48,628 | 50,002 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **2,649,438** | **2,552,480** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 278,678 | 310,033 |
| 18 | Amana za Wateja | 1,724,281 | 1,648,921 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 79,489 | 68,810 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 3,245 | 162 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 26 | 61 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 34,991 | 28,871 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 79,607 | 65,725 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 6,991 | 6,267 |
| 27 | Dhima Nyingine | 45,278 | 51,282 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **2,252,585** | **2,180,132** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **396,853** | **372,348** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 8,400 | 8,400 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 112,396 | 112,396 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 211,207 | 211,207 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 64,969 | 39,328 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | (119) | 1,017 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **396,853** | **372,348** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,142,674 | 861,303 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 56,148 | 56,197 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 59,265 | 56,896 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15.0% | 14.6% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.4% | 4.3% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 68.2% | 73.3% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 51.4% | 53.7% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 83.9% | 80.0% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 5.0% | 10.6% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 3.8% | 14.4% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA ILIYOISHIA 30 SEPTEMBA 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | TAARIFA | 30-Sep-23 | 30-Sep-22 | 30-Sep-23 | 30-Sep-22 |
| 1 | Mapato ya Riba | 49,683 | 31,426 | 131,908 | 87,117 |
| 2 | Gharama za Riba | 9,747 | 4,805 | 22,335 | 14,665 |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **39,935** | **26,621** | **109,573** | **72,452** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 3,567 | 701 | 5,935 | 8,761 |
| | **Mapato baada ya tengo katika mikopo** | 36,369 | 25,920 | 103,637 | 63,691 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **30,886** | **18,637** | **85,300** | **54,665** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 23,160 | 11,664 | 61,401 | 31,378 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 8,195 | 7,438 | 24,046 | 23,383 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | (469) | (464) | (148) | (96) |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba** | **30,917** | **27,979** | **92,992** | **81,239** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 18,024 | 16,446 | 55,451 | 48,400 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 737 | 1,980 | 2,036 | 6,763 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 12,157 | 9,554 | 35,505 | 26,076 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **36,337** | **16,577** | **95,945** | **37,117** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 10,697 | 5,411 | 30,977 | 11,946 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **25,641** | **11,167** | **64,969** | **25,171** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| | i) Mabadiliko ya thamani katika amana zinazouzika | (1,783) | (406) | (2,170) | (43) |
| | ii) Kodi ya mabadiliko ya thamani katika amana zinazouzika | 647 | 123 | 784 | (8) |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **24,505** | **10,884** | **63,583** | **25,120** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 590 | 542 | 590 | 542 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 3.1 | 1 | 7.7 | 3 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 14 | 14 | 14 | 14 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 4.0% | 2.2% | 3.6% | 1.7% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 26.4% | 13.1% | 23.3% | 10.0% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 43.7% | 61.8% | 47.7% | 63.9% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 7.4% | 6.1% | 7.6% | 5.7% |

*Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho*

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya sasa | Robo Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|---|
| | TAARIFA | 30-Sep-23 | 30-Jun-23 | 30-Sep-23 | 30-Sep-22 |
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **25,641** | **20,933** | **64,969** | 25,171 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 5,958 | 2,945 | 8,903 | 9,095 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 11,292 | (122,623) | (174,397) | (86,919) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | 14 | (11) | 2 | 503 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 68,567 | 312,725 | 442,029 | (105,126) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (37,300) | (82,607) | (92,317) | (36,004) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 23,243 | 6,741 | 42,319 | 30,191 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (3,732) | (9,928) | (15,590) | (19,602) |
| | - Kodi Iliyolipwa | (19,356) | (6,844) | (31,629) | (10,063) |
| | - Mengineyo (bainisha) | (14,342) | 1,648 | (10,060) | (12,868) |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **59,984** | **122,979** | **234,228** | **(205,622)** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (2,528) | (392) | (2,921) | (4,515) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 100 | 18 | 118 | 365 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(2,428)** | **(375)** | **(2,803)** | **(4,150)** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | (13,293) | (13,293) | (5,700) |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | (0) | (18,478) |
| | Mengineyo (bainisha) | - | 0 | - | 0 |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | - | (13,293) | (13,293) | (24,178) |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 57,556 | 109,311 | 218,132 | (233,951) |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 656,162 | 546,851 | 495,586 | 760,319 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 713,718 | 656,162 | 713,718 | 526,368 |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KILICHOISHIA 30 SEPTEMBA 2023
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mabadiliko thamani katika amana zinazouzika | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 8,400 | 112,396 | 224,500 | - | (0) | 1,267 | 346,563 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 64,969 | - | - | - | 64,969 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (1,386) | (1,386) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - 13,293 | - | - | - | (13,293) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,400** | **112,396** | **276,175** | **-** | **(0)** | **(119)** | **396,852** |
| 2 **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 8,400 | 112,396 | 203,613 | - | - 0 | 1,744 | 326,154 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 26,587 | - | - | - | 26,587 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | (477) | (477) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - 5,700 | - | - | - | (5,700) |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **8,400** | **112,396** | **224,500** | **-** | **- 0** | **1,267** | **346,563** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2023

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| Manzi Rwegasira<br>**(Mkurugenzi Mkuu)** | | 26-Oct-23 |
| Godwin Kapella<br>**(Kaimu Afisa Mkuu wa Fedha)** | | 26-Oct-23 |
| Jonathan Ngoma<br>**(Mkaguzi Mkuu wa Ndani)** | | 26-Oct-23 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| ***Jina*** | ***Saini*** | ***Tarehe*** |
|---|---|---|
| 1. Patrick Rutabanzibwa<br>**(Mwenyekiti wa bodi)** | | 26-Oct-23 |
| 2. Farzana Karimjee<br>**(Mjumbe wa bodi)** | | 26-Oct-23 |

TANGAZO

# BENKI YA STANBIC TANZANIA

## DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014

## MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

| No. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **1** | **CURRENT ACCOUNTS** | **TZS** | **USD** | **EUR** | **GBP** | **ZAR** |
| **a)** | **Required Minimum balance** | | | | | |
| | Personal Account | 10,000 | TZS EQV | TZS EQV | TZS EQV | TZS EQV |
| **b)** | **Monthly Service/Management Fees** | | | | | |
| | Personal Account | 3,000 | FREE | FREE | FREE | FREE |
| | Private banking PAYT | 29,500 | 17.70 | 14.16 | 10.62 | 164.02 |
| | Private banking Bundle | 53,100 | 31.86 | 24.78 | 18.88 | 295.00 |
| | Hekima | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| | Nyumbani (Diaspora) | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| | Biashara/Enterprise Direct | 15,000.01 | 10.62 | 8.26 | 7.08 | 97.94 |
| | SME banking (Commercial Tier 2) | 35,400 | 21.24 | 16.99 | 12.74 | 196.82 |
| | Commercial banking (Tier 1) | 64,900 | 38.94 | 30.68 | 23.60 | 361.08 |
| | Non commercial Entities | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| | Corporate & Investment Banking | 64,900 | 38.94 | 30.68 | 23.60 | 361.08 |
| **c)** | **Card & ATM fees** | | | | | |
| | Cash Withdrawal @ Branch Counter (Either With Cheque, Deposit Slip Etc.)-CURRENT ACCOUNT | TZS 6 500.01 for amounts below 20M, 0.1416% of value for amounts above 20M (max TZS 150 000) | 1.003% of value, min 8 | 1.003% of value, min 14.16 | 1.003% of value, min 14.16 | 1.003% of value, min 14.16 |
| | Cash withdrawal @ own ATM (in country) | 100,001 - 200,000 = 1,700<br>200,001 - 400,000 = 1,900<br>400,001 - 600,000 = 2,000.01 | 1.40 | 1.20 | 1.20 | 8.00 |
| | Cash withdrawal @ other bank ATM (in country) | 1,000 - 300,000 =2,800<br>300,001 - 400,000 =3,100<br>400,001-above=4,000 | 1- 170 =3<br>171-above=4 | 1- 170 =2.8<br>171-above=4 | 1- 170 =2.8<br>171-above=4 | 1- 2,000 =28<br>2,001-above=40 |
| | Cash withdrawal @ other bank ATM (international) | 9,000.01 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 53.34 |
| | Cash withdrawal @ own ATM (Cards from outside of Tanzania ) | 14,000 | TZS 14 000 EQV | TZS 14 000 EQV | TZS 14 000 EQV | TZS 14 000 EQV |
| | ATM card issuance | Classic- 5,000<br>Gold - 10,000<br>Platinum - 15,000.01 | TZS EQV | TZS EQV | TZS EQV | TZS EQV |
| | ATM card replacement/Renewal | 25,000.01 | 25.00 | 25.00 | 25.00 | 166.68 |
| | Annual card fees | Classic- 18,000<br>Gold - 24,000<br>Platinum - 48,000 | Classic- 8.00<br>Gold - 10.00<br>Platinum - 30.00 | Classic- 8.00<br>Gold - 10.00<br>Platinum - 30.00 | Classic- 8.00<br>Gold - 10.00<br>Platinum - 30.00 | Classic- 50.00<br>Gold - 66.67<br>Platinum - 200.00 |
| **d)** | **Account Statements** | | | | | |
| | Mini Statement (own ATM) | 900.01 | 0.91 | 0.91 | 0.91 | 6.01 |
| | Interim Statement per page over the counter | 5,000 | 5 | 5 | 5 | 33.34 |
| | Periodic schedule statement | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| | History statements over the counter | 60,000 | 31.00 | 31.00 | 26.00 | 400.01 |
| | Balance enquiry (Own ATM) | 500 | 0.31 | 0.31 | 0.31 | 2.01 |
| | Balance enquiry (Over the counter) | 2,500 | TZS EQV | TZS EQV | TZS EQV | TZS EQV |
| **e)** | **Over the Counter Transactions** | | | | | |
| | Issue of cheque book (per leaf) | 450 | 0.46 | 0.46 | 0.46 | 3.01 |
| | Returned unpaid Cheque( insuficient fund) | 100,000.01 | 100.01 | N/A | N/A | N/A |
| | Counter Cheque | 15,000 | 15.00 | 15.00 | 15.00 | 100.00 |
| | Stop Payment | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| | Cheque Deposit | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| | Cash Deposit | FREE | 1.77% of notes below $50 | FREE | FREE | FREE |
| **2** | **SAVINGS ACCOUNTS** | **TZS** | **USD** | **EUR** | **GBP** | **ZAR** |
| **a)** | **Required minimum opening & operating balance** | | | | | |
| | Hatua Savings | 5,000 | 10 | N/A | N/A | N/A |
| | Pure Savings | 50,000 | 100 | 100 | 100 | 300 |
| **b)** | **Monthly service fee<br>(if balance breach minimum balance required)** | | | | | |
| | Hatua Savings | 1,999.99 | 1.00 | N/A | N/A | N/A |
| | Pure Savings | 1,999.99 | 1.18 | 1.18 | 1.18 | 17.70 |
| **c)** | **ATM fees** | | | | | |
| | Cash Withdrawal @ Branch Counter- Hatua Savings (Free-once per month) | 10,000 for amounts below 20M, 0.14 % of value max for amount above 20M (max 118,000) | 1.18 % min 10 | N/A | N/A | N/A |
| | Cash Withdrawal @ Branch Counter -Pure Savings (Free-once per month) | 5,900 for amounts below 20M, 0.14 % of value for amount above 20M (max 118,000) | 1.18 % min 10.62 | 1.18% min 21.24 | 1.18% min 21.24 | 1.18% min 212.4 |
| **d)** | **Interim statement** | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| **e)** | **Account closure** | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| **3** | **ELECTRONIC BANKING (Internet & Simbanking)** | **TZS** | **USD** | **EUR** | **GBP** | **ZAR** |
| **a)** | Internet transfers own account & 3rd party within Stanbic | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| **b)** | Internet transfers other banks (EFT) | 2,000.01 | 2.01 | 2.01 | 2.01 | 13.33 |
| **c)** | Internet transfers other banks (TISS) | 8,000.01 | 3.47 | 3.10 | 2.67 | 50.11 |
| **d)** | Mobile top up | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| **e)** | Bank to wallet | 0-10,000 = 1,100<br>10,001-20,000 = 2,500<br>20,001-30,000 = 3,300<br>30,001-50,000 = 3,500<br>50,001-100,000 = 4,770<br>100,001-200,000 = 5,400<br>200,001-300,000 = 6,000.01<br>300,001-400,000 = 6,500.01<br>400,001-500,000 = 7,000<br>500,001-700,000 = 8,100<br>700,001-800,000 = 8,600.01<br>800,001-1,000,000 = 9,500<br>1,000,001-2,000,000 = 10,500.01 | N/A | N/A | N/A | N/A |

| No. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **4** | **PAYMENTS & TRANSFERS** | **TZS** | **USD** | **EUR** | **GBP** | **ZAR** |
| **a)** | Salary payment to staff banking with other bank (EFT) | 5000 | 5.00 | 5.00 | 5.00 | 33.34 |
| **b)** | Salary payment to staff banking with other bank (TISS) | 10,000 | 4.47 | 3.63 | 3.47 | 60.22 |
| **c)** | Standing Order to 3rd party within stanbic | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| **d)** | Standing Order to other banks local | 40,000.01 | 40.00 | 40.00 | 40.00 | 266.67 |
| **e)** | Standing Order own account | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| **f)** | Transfers through TISS (Outward) | 11,800 | TZS EQV | TZS EQV | TZS EQV | TZS EQV |
| **g)** | Transfers through TISS (Inward) | FREE | FREE | FREE | FREE | FREE |
| **5** | **FOREIGN FUNDS TRANSFERS** | **TZS** | **USD** | **EUR** | **GBP** | **ZAR** |
| **a)** | Purchase of foreign cheque | 1.18% of the amount min 100 000, Max 400 000 | 1.18% of the amount min 59, Max 236 | 1.18% of the amount min50, Max 200 | 1.18% of the amount min 40, Max 160 | 1.18% of the amount min 560, Max 2240 |
| **b)** | Telegraphic transfer Inward | $10 (across all currencies) | | | | |
| **c)** | Telegraphic transfer Outward (BEN/OUR/SHAR) | 0.3%. of value, Min $50, Max $150 (excluding overseas charge across all currencies) | | | | |
| **d)** | Overseas charges | $29.5 (across all currencies) | | | | |
| **e)** | Cancellation of TT/Recall of funds | $75 (across all currencies) | | | | |
| **6** | **TRADE FINANCE** | **TZS** | **USD** | **EUR** | **GBP** | **ZAR** |
| **a)** | **Letters of Credit/Guarantee** | | | | | |
| | Establishment/Re-issuance | USD EQV | 1% per quarter, min 300 | USD EQV | USD EQV | USD EQV |
| **b)** | **Documentary collection( clean bill)** | | | | | |
| | Advising/Handling commission | $150 | 150 | USD EQV | USD EQV | USD EQV |
| **7** | **LOANS** | **TZS** | **USD** | **EUR** | **GBP** | **ZAR** |
| **a)** | Processing/ Arrangement/ Appraisal fee | | | | | |
| | (i) Personal Loans | 2.00% | 2.00% | | | |
| | (ii) Overdrafts | 1.5% of the facility min 50 000. | 1.5% of the facility min $50 | | | |
| | (iii) Mortgage Finance | 1.00% | 1.00% | | | |
| | (iv) Asset Finance | 1.18% | 1.18% | | | |
| | (v) Facilitation of Loan Amendments | | 750 | | | |
| **b)** | Early repayment (full settlement) | 8% of outstanding balance | 8% of outstanding balance | | | |
| **c)** | Valuation fees | As per valuer | As per valuer | | | |
| **8** | **LENDING RATES** | **TZS** | **USD** | **EUR** | **GBP** | **ZAR** |
| | Base/Prime Lending Rate | 21% | 13.5% | | | |
| **9** | **DEPOSIT RATES (*subject to change from time to time*)** | **TZS** | **USD** | **EUR** | **GBP** | **ZAR** |
| **a)** | Fixed Deposits | | | | | |
| | **Tenure** | **+1BN** | **+1M** | | | |
| | 1month | 1.75% | 0.20% | | | |
| | 3months | 2.50% | 0.25% | | | |
| | 6months | 3.50% | 0.45% | | | |
| | 9months | 4.00% | 0.55% | | | |
| | 12months | 4.75% | 0.60% | | | |
| **b)** | Savings Deposits | 3.00% | 0.20% | | | |
| **10** | **EAST AFRICA BORDERLESS BANKING** | **(KES,TZS,UGX)** | **USD** | **EUR** | **GBP** | **ZAR** |
| **a)** | Cash withdraw over the counter | KES 200, TZS 5 000, UGX 10 000 | 3.00 | 3.00 | 3.00 | $1.8 EQV |
| **b)** | Cash deposit over the counter | FREE | FREE | FREE | FREEE | FREE |
| **11** | **TREASURY BILLS & BONDS** | **TZS** | **USD** | **EUR** | **GBP** | **ZAR** |
| **a)** | Bonds and Bills purchase fees | 75,000 for purchases of TZS 1M to TZS 250M & 100,000 for purchases greater than TZS 250M | | | | |

**We, the undersigned have examined the information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.**

| Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|
| Manzi Rwegasira | Chief Executive Officer | | |
| Omari O Mtiga | Head, Personal & Private Banking | | |
| Fredrick Max | Head, Business & Commercial Banking | | |

**FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED** First Housing

**FIRST HOUSING FINANCE (TANZANIA) LIMITED** commenced its operations in October 2017 as a fully-fledged financial institution specializing on the provision of residential mortgages. The company was licensed by Bank of Tanzania in July 2017 to commence housing finance business under the provisions of The Banking and Financial Institutions Act, 2006 (Cap. 342. R.E. 2002).

We are looking to hire competent and skilled Relationship Officers to join our team. If you're confident that you possess strong problem solving skills, excellent communicator, good at sales and marketing, good rapport with customers and a strategic thinker along with analytical mind, First Housing Finance is a great place for you to grow your career.

As Relationship Officer you shall be responsible with overall facilitation of company mortgage business growth and increase in sales volumes by developing and implementing comprehensive marketing and sales plans that promote company's brand awareness, brand recognition and brand loyalty for our company's gaining a competitive advantage in the mortgage market.

| | | |
|---|---|---|
| **Job Title** | : | **Relationship Officers (2 Positions)** |
| **Reporting to** | : | **Business Manager** |
| **Location** | : | **Dar Es Salaam** |

**Duties & Responsibilities – Relationship Officer**

- Plan for sales activities on a Daily and weekly basis making visits to targeted customers & prospects in line with FHF sales practices and guidelines and ensures sales leads optimization;
- Market the Home Loans products to increase the Loan book in line with the Company budgeted weekly and monthly targets;
- Identify & acquire home loan pipeline applicants in line with Company's policies;
- Marketing FHF social media accounts and ensure are updated on daily basis;
- Ensuring graphic designed artworks are well used in different events as per marketing calendar;
- Prepare a weekly report based on the sales activities, analyzing with Business Manager the achievements, variances and planning for corrective actions in case of variances
- Building relationships with existing customers in order to pro-actively anticipate and address future customer needs and identify sales opportunities Undertake in-branch marketing, special campaigns, and promotions
- Develop builder corporate network to source best in class customer profiles, business leads and engagements;
- Communicate effectively with clients to understand specific needs and help the credit team to structure the mortgages to the best possible offer in line with cash flows.
- Understand Company's various policies and more importantly the AML Policy, KYC policy and mortgage policy as well as regulators various laws, regulation and guidelines;
- Liaising and networking in the industry to seek reference checks for clients as well as understanding the industry & economic dynamics;
- Ensuring adherence to company sourcing, credit &operational policies
- Manage credit quality and control delinquencies, frauds;
- Ensuring and monitoring that external regulations of lending as and when updated by various institutions are not violated;
- Well versed with property (land/ house/ apartment) related legal & technical requirements
- Own and manage customer queries and complaints by taking ownership and resolving in a timely manner
- Updated with all relevant real estate developments and all mortgage chain value;
- Manage the process required for delivering reasonable turnaround time;
- Provide superior customer experience through courteous handling and effective service.
- Deliver world class customer relationship management practices and ensure adherence to First Housing Finance Service standards and code of conducts
- Monitor and follow up your mortgage portfolio to identify deteriorating credit situations, take appropriate action to address the problem mortgages.
- Any other duties and responsibilities as you may be assigned by your supervisors.

**EXPERIENCE, QUALIFICATIONS& COMPETENCIES**

- University degree or advanced diploma in Business Administration, Banking, Finance or related field.
- At least 5 years' practical experience in a Financial industry especially on credit functions or Mortgage financing.
- Communication and influencing skills, involving staff at all levels of seniority
- Facilitation skills
- Analytical and problem solving skills
- Service excellence
- Good time management and organizational skills
- Team player

**Applications: Qualified candidates to Send CV and application letter to:info@firsthousing.co.tz**

**Deadline: 03rd November 2023.**

217672101

# Watanzania wenye kipato cha chini kuwezeshwa kumiliki nyumba bora

**Na Romana Mallya**

KATIKA jitihada za kupanua na kuimarisha upatikanaji wa nyumba bora na za bei nafuu, Kampuni ya Tanzania Mortgage Refinance (TMRC) imezifikia benki 18 kuwa wanahisa ili Watanzania wenye kipato cha chini kuwezeshwa kuwa na nyumba bora na za bei nafuu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TMRC, Oscar Mgaya, aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wakimkaribisha mwanahisa mpya Benki ya Mwanga Hakika, ambaye amewekeza mtaji wa Sh. milioni 500 ili kutoa mikopo ya nyumba kwa wananchi.

Alisema takwimu zinaonyesha kuna ongezeko la uhitaji wa nyumba 200,000 kila mwaka nchini huku taifa likiwa linakibiliwa na upungufu wa nyumba za makazi milioni tatu.

Mgaya alisema hatua hiyo iliyofikiwa itaisaidia benki hiyo ambayo sasa imekuwa mwanahisa wa 18 TMRC, kutoa mikopo ya nyumba ya muda mrefu na nafuu kwa wananchi wanaohitaji.

"Kama mkopeshaji wa jumla, tunataka kuendelea kupanua huduma zetu ili kuzifikia benki na taasisi nyingi za fedha ili kuwawezesha Watanzania kuendelea kupata makazi bora. Toka tumeanza kwenye soko letu tuna benki 31 zinazotoa mikopo ya nyumba," alisema.

Aidha, alisema mahitaji ya sekta ya nyumba yanayokua kwa kasi yanachangiwa zaidi na ukuaji wa uchumi imara na endelevu huku Pato la Taifa ikiwa wastani wa asilimia sita hadi saba katika muongo mmoja uliopita.

Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Mwanga Hakika, Jagjit Singh, aliishukuru TMRC kwa kuwakaribisha ili kusaidia zaidi kupanua upatikanaji wa mikopo ya nyumba kwa Watanzania.

# Nguzo za asili zagundulika Hifadhi ya Taifa Ruaha

**Na Mary Geofrey**

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa (TANAPA) katika kuongeza mazao mapya ya utalii, limegundua eneo jipya lenye hazina kubwa ya nguzo za asili zenye mwonekano wa kuvutia ndani ya Hifadhi ya Taifa Ruaha.

Nguzo hizo zilizosimama mithili ya uyoga na kuvutia kwa macho zinasemekana zimetokana na kumomonyoka kwa miamba yenye sifa tofauti kunakosababishwa na mtiririko wa maji na upepo.

Kamishna Msaidizi Mwandamizi na Mkuu wa Hifadhi ya Taifa Ruaha, Godwell Meing'ataki, alibainisha hayo juzi alipozungumzia kivutio hicho kipya cha utalii.

"Kwa mara ya kwanza tukiwa tunashuka na helikopta katika eneo hili, tulishangazwa na wingi wa nguzo hizi za asili na tukajua ndio hazina pekee iliyopo hapa, lakini tulipolizunguka eneo hili tuligundua lina utajiri mwingine wa masalia ya zana za mawe mithili ya zile zilizotumika nyakati za zama za mawe za mwanzo," alisema.

Zana zinazoonekana katika eneo hilo jipya ni pamoja na mawe magumu yaliyotumiwa na binadamu wa mwanzo kusaga nafaka kwa ajili ya chakula au mizizi na magome ya miti kwa ajili ya tiba asilia, miamba iliyochongwa kiustadi mithili ya mikuki, mashoka na zana nyingine zilizotumika katika shughuli za uwindaji.

Alisema mwenye kumbukumbu na ufahamu wa nguzo za asili na zana za mawe zilizomo nchini, anaweza kudhani ni Isimila ilhali ni moja ya maeneo yaliyomo ndani ya Hifadhi ya Taifa Ruaha, takribani Km 70 kutoka makao makuu ya hifadhi hiyo yaliyoko Msembe.

"Kwa utajiri wa nguzo, zana za mawe pamoja na sifa nyingine kedekede, eneo hili linakidhi vigezo vya kuwa Geopark. Kama tunavyofahamu Bara letu la Afrika lina Geopark mbili tu, lakini tunashukuru ndani ya Hifadhi ya Taifa Ruaha tuna eneo linaloweza kukidhi vigezo hivyo, likikidhi vigezo litatoa fursa kwa hifadhi hii kutambulika zaidi kimataifa tofauti na ilivyo sasa," alisema Kamishna Meing'ataki.

Alisema jitihada za kulitangaza eneo hilo zimeanza ndani na nje ya mipaka ya Tanzania ili kuvutia watalii wengi zaidi na wawekezaji, ikizingatia kuwa ni kivutio kipya na muhimu kwa watalii wanaotembelea Hifadhi ya Taifa Ruaha na hifadhi zingine zilizoko ukanda wa kusini.

Kamishna Meing'ataki aliongeza: "TANAPA itafanya taratibu za kuwaalika watafiti mbalimbali wa miamba, udongo na malikale wa ndani na nje kubaini na kupata taarifa sahihi za malikale zilizopo, taarifa ambazo zitalitambulisha eneo hili kimataifa."

Kutokana na unyeti wa eneo hilo, Menejimenti ya Hifadhi ya Taifa Ruaha imefanya jitihada za kutengeneza barabara ili eneo hilo lifikike kiurahisi hasa kipindi hiki ambacho watalii wengi wana shauku na bashasha ya kwenda kulitembelea na kuziona nguzo na zana hizo.

"Uimarishaji barabara unakwenda sambamba na tathmini za kiutalii, kiikolojia na ulinzi kubaini maeneo muhimu yatakayojengwa miundombinu ya kiutalii ili wageni wanapotembelea eneo hilo wapate huduma ya malazi na chakula.

"Hatua hizi zikikamilika zitavutia watalii wengi na siku za kukaa hifadhini zinatarajia kuongezaka, siku zikiongezeka na mapato yanaongezeka kwa taifa," alisema Meing'ataki.

Nipashe

IJUMAA OKTOBA 27, 2023

BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akiwa kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa. **PICHA: MTANDAO.**

# Rasmi Dk. Samia kauingiza mchezo 'soka' katika Diplomasia Uchumi

**Na Peter Orwa**

WIKI hii Rais Dk. Samia Suluhu Hassan amekuwa nje ya mipaka jijini Lusaka, katika ujirani mwema wa Siku ya Uhuru wa Zambia.

Kama ilivyo kawaida yake, ni tukio lililoendana na kuboresha undugu wa uhusiano kibiashara, kutiwa saini mikataba ya makubaliano ya mambo manane.

Vilevile, Rais Hakainde Hichilema, akawapa ofa Watanzania kuingia nao ushirikiano wa kilimo, ikizingatiwa nchi yao sasa inang'ara na imenuia kwa hatua zake.

Kimsingi, staili za Rais Dk. Samia, tangu kuingia madarakani, amekuwa anajenga hamasa za kiuchumi katika sekta mbalimbali, ikiwamo kilimo ikifungua sura ya ukuaji kibiashara na sekta nyinginezo.

**MICHEZO NA BURUDANI**

Sekta michezo, ambako imedumu miaka mingi kuwa ya burudani, nayo sasa inaangukia sura ya uchumi, katika dhana kuwa na msisitizo wake Rais Dk. Samia tangu anaingia madarakani; utalii uwe na mawanda mapana, yeye akionyesha mfano kuongoza filamu maalum yenye tija na matokeo chanya.

Ni tafsiri inayoendana na sekta hizo, michezo na burudani huku nayo ikivutia kimataifa, hata kukaribisha wageni huku nayo ikichangia uchumi wa taifa.

Hapo akatumia kanuni inayotumika kiuchumi, kibiashara na kifedha kwamba namna unavyowekeza zaidi ndio kunavyotoa matunda ya faida maradufu.

Kimsingi, michezo na burudani ni aina ya mifumo ambayo matunda yake yanategemea zaidi katika uwekezaji wa nguvu kazi inayozalisha matunda katika sekta hiyo.

Inaeleweka, tayari hali ya ushindani katika soka la nchi ilishaanza kuchukua hatua, hata nchi inang'ara zaidi katika ukanda Afrika Mashariki na Kati na imevuka mipaka.

Pia, kwenye serikali ya Awamu ya Tatu chini ya Rais Benjamin Mkapa, kukajengwa uwanja ambao sasa una heshima kubwa ndani ya Bara Afrika; Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Rais Dk. Samia akaamua kuhamasisha michezo kiuchumi, kwa kuwekeza hamasa kwa washiriki pale wachezaji timu ya wanawake Twiga Stars.

Pia, ana uwekezaji wa pili ukawa pale alipohamasisha makubwa katika soka nchini, akiahidi mathalan tukio la kwanza akianza na kutoa shilingi milioni tano kwa kila goli linalofungwa mchezoni.

Hiyo ni katika matukio tofauti ambayo yamehusu timu za Simba, Yanga, Azam na Singida Stars na Timu ya Taifa au Taifa Stars katika mechi za kimataifa.

Ni siku chache zilizopita, kati ya wiki hii na mwishoni mwa wiki iliyopita, wakati timu ya Simba, katika mechi zake ngazi za robo fainali barani Afrika dhidi ya Al Ahly, Rais akaahidi kutoa shilingi milioni 10 kwa kila goli, iwapo ingeshinda.

Simba ilitolewa katika michuano hiyo, kwa kuzidiwa idadi ya magoli, huku ikionyesha kiwango kikubwa, licha kutoka sare Dar es Salaam na jijini Cairo, Misri.

Hayo yanatokea, huku kukishuhudiwa mapinduzi makubwa kwenye ulingo wa soka nchini, soka la wanawake likionesha makubwa, timu ya taifa kufuzu ngazi ya juu kimataifa.

Vyote vinajionyesha zao la mustakabali wa kazi ya kiutawala kutoka kwa Rais Dk. Samia, akiwekeza katika michezo na matunda yake kujionesha.

Licha ya uwekezaji fedha katika eneo hilo, Dk. Samia pia hakukaa nyuma, mbali na kutoa taarifa za kimichezo, anakuwa akijitokeza uwanjani mgeni rasmi, hata kutoa hamasa kubwa katika ukuaji wake.

Hilo limeendana na matukio kadhaa, akialika vilabu vya mchezo wa soka kwenda kwenye chakula cha jioni, Ikulu mambo ambayo yamekuwa hamasa kubwa katika ukuaji michezo nchini.

Moja ya matukio ambayo sasa yanaweka historia ya nchi, ni pale alipoamua katika matukio kutoa ndege ya serikali kutumiwa vilabu vya michezo kwa safari za nje na ndani, hapo wanufaika wakiwamo mabingwa wa soka nchini, klabu ya Yanga, pia Timu ya Taifa ya Wanawake.

Hiyo inajitokeza hata katika bajeti ya serikali, hivi sasa katika uongozi wa Dk. Samia inatajwa Sekta ya Michezo na Burudani inatengewa kiwango kikubwa zaidi, hata sekta inajimudu maradufu.

Pia, katika moja ya uamuzi kifedha, Rais Dk. Samia akaamua kuwekeza katika michezo na burudani, serikali ikichukua jukumu la kukarabati viwanja vingi nchini, moja ya zao lake ni ukarabati mkubwa wa Uwanja wa Taifa wa Dar es Salaam, ambako kukatengwa wastani wa fungu shilingi bilioni 31 ya kuukarabati.

Ni uamuzi wa aina hiyo ukachukua sura katika maboresho ya viwanja katika mikoa mbalimbali nchini, vinavyomilikiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM), ila vinatumika katika ligi ya soka nchini, michezo, burudani, pia matukio mbalimbali kitaifa.

Vilevile kunahesabika wiki kadhaa, Tanzania iliomba na kukubaliwa kuwa mwenyeji wa Michuano ya Soka Mtaaifra ya Afrika (AFCON) mwaka 2027, sasa ikiwa katika mchakato wa kutimiza sharti la ujenzi wa viwanja vipya vitatu vyenye uwezo wa kuchukua watazamaji 30,000 kila kimoja, katika mikoa ya Mwanza, Dodoma na Arusha, kutumika kwa michuano hiyo.

Kwa kifupi, hatua za maboresho hayo yameleta mageuzi makubwa sasa Tanzania inatumika sana kimataifa katika ulimwengu wa soka duniani.

Ikadhihirika hivi karibuni, baada ya kufunguliwa Uwanja wa Taifa, mchezo wa kimataifa baina ya Simba na Al Ahly ya Misri, kukawapo ugeni rasmi wa Rais wa Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), Gianni Infantino, mjumbe wake, Arsene Wenger, pia Moise Katumbi, ambaye ni mmiliki wa klabu ya soka ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidermokrasi ya Congo (DRC).

Siku chache baada ya kuondoka nchini, viongozi hao wa soka kimataifa wakamsifu mwenyeji wao Rais Dk. Samia kwa uwekezaji mkubwa uliofanywa katika soka nchini.

Hilo linafanyika, huku timu ya soka ya DRC ikiomba kutumia Uwanja wa Uhuru kwa mechi zake, jambo ambalo ni la ushindi mkubwa kiuchumi kitaifa, ikizingatiwa uwanja huo unakodiwa kwa kiasi cha shilingi milioni 20 kwa kila mechi.

Ni hali inayothibitisha utalii wa michezo na burudani umeanza nchini, ugeni mkubwa wa michezo kimataifa ukikaribisha mengi kiuchumi, mapato katika maeneo kama ya viwanja, usafiri, mlo na pa kulala.

Vilevile, ni eneo la kisekta limeongeza mzunguko wa kifedha na biashara nchini, ikipanua wigo wa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja, ndani ya sekta hiyo ukiwa na ushindani mkubwa kitaifa, unaaza ajira ya wanamichezo na wale wanaowahudumia kama madaktari.

Wizara mama ya Michezo, Rais Dk. Samia ameimarisha muundo wake ikibaki zaidi na michezo na burudani, habari iliyokuwapo zamani, imetenganishwa katika wizara tofauti, sasa Waziri wake ni Dk. Damas Ndumbaro, naye anajulikana ni mpenzi mkubwa wa michezo na hasa soka nchini. Ni rasmi, Tanzania chini ya Rais Dk. Samia, imeingiza michezo katika Diplomasia Uchumi.

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA
## Imetolewa chini ya Kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

Amana Bank
*Pamoja, katika njia sahihi*

**WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023**

| | SHS '000 Robo Mwaka/ Mwaka wa sasa 30 - 09 - 2023 | SHS '000 Robo Mwaka iliopita 30 - 06 - 2023 |
|---|---|---|
| **A. MALI** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 17,656,162 | 20,030,798 |
| 2. Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 30,544,544 | 25,454,749 |
| 3. Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 0 | 0 |
| 4. Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 4,924,211 | 6,061,330 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 151,588 | 208,950 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 40,733,578 | 34,696,504 |
| 10. Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 1,000,479 | 1,044,110 |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 166,944,502 | 168,607,885 |
| 12. Mali Nyingine | 9,681,863 | 10,258,250 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14. Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 9,066,219 | 9,429,771 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **280,703,146** | **275,792,348** |
| | | |
| **B. DHIMA** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 8,238,200 |
| 18. Amana za Wateja | 226,918,517 | 205,348,958 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20. Amana Maalumu | 12,293,107 | 17,236,356 |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 153,552 | 160,024 |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,825,678 | 2,379,280 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 17,480 | 20,410 |
| 27. Dhima Nyingine | 7,653,561 | 9,962,012 |
| 28. Madeni | 6,750,000 | 6,750,000 |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | 256,611,895 | 250,095,239 |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **24,091,251** | **25,697,109** |
| | | |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 45,060,215 | 45,060,215 |
| 32. Akiba ya Mtaji | 0 | 1,802,537 |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (19,864,455) | (21,666,992) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (1,104,509) | 501,349 |
| 35. Akaunti Nyingine za Mtaji | 0 | 0 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **24,091,251** | **25,697,109** |
| | | - |
| 38.Dhima Zisizo Dhahiri | 5,375,440 | 6,628,530 |
| 39. Mikopo Chechefu | 10,874,483 | 16,828,362 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 6,678,301 | 5,577,449 |
| 41. Mali Nyingine Chechefu | 0 | 0 |
| | | |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9% | 9% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 6.2% | 9.6% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 73% | 75% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 62% | 63% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 77% | 76% |
| (vi) Ongezeko la Amana | 4% | 9% |
| (vii) Ongezeko la Mali | 1.8% | 8% |

**TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2023**

| | SHS'000 Robo ya Mwaka sasa | SHS'000 Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | SHS'000 Limbikizo la Mwaka wa sasa | SHS'000 Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|
| | **30 - 09 - 2023** | **30 - 09 - 2022** | **30 - 09 - 2023** | **30 - 09 - 2022** |
| 1. Faida itokanayo na Mikopo | 5,938,129 | 4,332,364 | 15,853,777 | 12,259,340 |
| 2. Gawio la Faida kwa waweka Amana | (440,681) | (458,850) | (1,445,728) | (1,341,784) |
| 3. Mapato Halisi ya Faida (1kutoa 2) | 5,497,448 | 3,873,514 | 14,408,049 | 10,917,556 |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | (2,848,176) | 8,168 | (2,567,692) | -87,538 |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (413,999) | 0 | (1,440,057) | 409,405 |
| | | | | |
| **6. Faida isiyotokana na Mikopo:** | **1,842,061** | **1,737,745** | **5,677,978** | **5,006,205** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 386,039 | 315,563 | 912,843 | 957,255 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 1,456,022 | 1,422,182 | 4,765,135 | 4,048,950 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **7. Gharama za uendeshaji:** | (5,240,220) | (4,947,569) | (15,853,873) | (14,657,080) |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (2,404,405) | (2,082,037) | (7,152,245) | (6,021,756) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (2,835,814) | (2,865,531) | (8,701,628) | (8,635,324) |
| 8. Faida /(Hasara) ya Uendeshaji | (1,162,886) | 655,522 | 224,406 | 944,814 |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | (442,972) | (27,205) | (1,328,915) | (81,616) |
| **10. Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | (1,605,858) | 628,317 | (1,104,509) | 863,198 |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,605,858)** | **628,317** | **(1,104,509)** | **863,198** |
| | | | | |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 321 | 270 | 321 | 246 |
| 14. Mapato kwa Hisa | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 15. Idadi ya Matawi | 10 | 10 | 10 | 10 |
| | | | | |
| BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -2.31% | 2.49% | -1.59% | 3.43% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -18% | 4% | -18% | 4% |
| (iii) Uwiano wa Gharama za uendeshaji na Mapato Ghafi | 67% | 82% | 67% | 102% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya yatokanayo na Mikopo na Wastani wa Mali | 9% | 2% | 9% | 6% |

**TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2023**

| | SHS'000 Robo Mwaka Mwaka wa sasa 30 - 09 - 2023 | SHS'000 Robo Mwaka Uliopita 30 - 06 - 2023 |
|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (1,605,858) | 179,743 |
| Marekebisho kwa Ajili ya | - | - |
| - Uchakavu Katika Mali | 3,876,991 | 1,300,870 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| - Gharama za ukodishaji | 153,861 | 153,861 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 562,532 | (11,136,294) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 8,388,110 | 19,521,614 |
| - Mabadiliko ya kiwango kinachohitajika na banki kuu kisheria | (946,696) | (887,110) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (2,665,221) | 824,710 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (576,387) | (154,565) |
| - Mengineyo (bainisha) | - | - |
| - Kodi Iliyolipwa | (33,122) | (33,122) |
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | 7,154,210 | 9,769,706 |
| | - | - |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaj** | - | - |
| Gawio Lililopokewa | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (61,121) | (118,646) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (64,479) | (68,938) |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Marekebisho katika mali za Kudumu | - | - |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji | (125,600) | (187,584) |
| | - | - |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha** | - | - |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (403,823) | (403,823) |
| Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | (403,823) | (403,823) |
| | - | - |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | - | - |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 6,624,787 | 9,178,300 |
| | - | - |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu kwa Mwanzo wa Robo ya Mwaka | 73,763,351 | 64,585,051 |
| | - | - |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo ya Mwaka** | **80,388,138** | **73,763,351** |

**TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2023**

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyo-bakizwa | Ziada ya Kisheria | Mengi-neyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa 2023 | | | | | | |
| | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 45,060,215 | 0 | (21,066,440) | 1,201,985 | 0 | 25,195,760 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (1,104,509) | 0 | 0 | (1,104,509) |
| Share zilizouzwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 1,201,985 | (1,201,985) | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la Robo ya mwaka** | **45,060,215** | 0 | **(20,968,964)** | - | 0 | **24,091,251** |
| | | | | | | |
| Mwaka Uliopita 2022 | | | | | | |
| | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa Mwaka | 42,006,260 | 0 | (24,662,883) | 3,941,327 | 0 | 21,284,704 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 857,101 | 0 | 0 | 857,101 |
| Share zilizouzwa | 3,053,955 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3,053,955 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Gawio lililolipwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | 2,739,342 | (2,739,342) | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **45,060,215** | 0 | **(21,066,440)** | **1,201,985** | 0 | **25,195,760** |

Katika kuanda taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

Jina na cheo

**Musa Kitoi**
(Naibu Mkurugenzi Mtendaji) — Imesainiwa Oktoba 26, 2023

**CPA Saidi Mbaruku**
(Mkuu wa fedha) — Imesainiwa Oktoba 26, 2023

**CPA Mwinyi Sekro**
(Mkuu wa Ukaguzi) — Imesainiwa Oktoba 26, 2023

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

**Joseph Gonsalves**
(Mwenyekiti) — Imesainiwa Oktoba 26, 2023

**Salem Balleith**
(Mkurugenzi) — Imesainiwa Oktoba 26, 2023


UWEZESHAJI *kwa wastaafu*

Kwa Wastaafu Wanaostahiki wa PSSSF, HAZINA, NSSF & ZSSF

Amana Bank
*Pamoja, katika njia sahihi*




TANGAZO

TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC TACOBA "Our Bank for Our Development"

# BENKI YA WANANCHI TANDAHIMBA

## UONYESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha '(Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE - 30 SEPTEMBA, 2023

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo mwaka ya sasa 30/09/2023 | Robo mwaka iliyopita 30/09/2023 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1. | Fedha Taslimu | 8,101 | 19,310 |
| 2. | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | - | - |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 752,683 | 824,167 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 3,030,268 | 2,693,911 |
| 12 | Mali Nyingine | 178,712 | 132,622 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za Udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 156,990 | 168,045 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **4,126,754** | **3,838,054** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | - |
| 18 | Amana za Wateja | 871,986 | 1,064,847 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo /Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 63,010 | 45,936 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | 104,180 | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 30,342 | 14,994 |
| 28 | Madeni | 797,813 | 500,000 |
| 29 | **JUMLA YA DHIMA** | **1,867,331** | **1,625,777** |
| 30 | **MALI/ DHIMA HALISI (16 kutoa 29)** | **2,259,423** | **2,212,277** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 4,483,228 | 4,483,228 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yalibakizwa | (2,348,098) | (2,333,725) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (11,172) | (58,319) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 135,465 | 121,093 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **2,259,423** | **2,212,277** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo Chechefu | 56,259 | 243,517 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 35,116 | 65,204 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 54.8% | 57.6% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.8% | 8.8% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi Halisi na Jumla ya Amana | 351.5% | 259.1% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 73.4% | 70.2% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 91.7% | 91.7% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -18.1% | 45.0% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 7.5% | 9.4% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA - 30 SEPTEMBA, 2023

| | | Robo mwaka ya sasa 30/09/2023 | Robo mwaka Iliyopita 30/09/2022 | Mwaka wa Sasa 30/09/2023 | Mwaka Uliopita 30/09/2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mapato ya Riba | 166,239 | 125,444 | 384,476 | 412,838 |
| 2. | Gharama za Riba | (21,815) | (7,874) | (54,336) | (25,273) |
| 3. | **Mapato Halisi ya Riba ( 1 kutoa 2)** | **144,424** | **117,570** | **330,140** | **387,565** |
| 4. | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 33,498 | 174 | 44,348 | 12,817 |
| 6. | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **26,667** | **55,387** | **92,972** | **145,953** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | - | - | - | - |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 26,667 | 55,387 | 92,972 | 145,953 |
| | 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | - | - | - | - |
| 7. | **Gharama Zisizo za Riba** | **(157,443)** | **(171,438)** | **(478,633)** | **(477,366)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (47,352) | (55,825) | (160,906) | (182,767) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (110,091) | (115,613) | (317,727) | (294,599) |
| 8. | **Faida / (Hasara) Halisi ya Uendeshaji** | **47,146** | **1,693** | **(11,172)** | **68,968** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | (508) | - | (24,498) |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **47,146** | **1,185** | **(11,172)** | **44,470** |
| 11 | Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| 12 | Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka | 47,146 | 1,185 | (11,172) | **44,470** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 16 | 15 | 14 | 13 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 11 | (2) | (2) | 10 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| | (i)Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 4.6% | -0.3% | -0.4% | 3.0% |
| | (ii)Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 8.2% | -0.5% | -0.7% | 2.6% |
| | (iii)Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 92.0% | 96.3% | 113.1% | 89.5% |
| | (iv)Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 17.3% | 8.1% | 13.0% | 17.9% |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA,2023**

**Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita**

| | Tarehe | Saini |
|---|---|---|
| Yahya J. Kiyabo<br>**Meneja Mkuu** | 25/09/2023 | |
| Julius J. Sawaya<br>**Mkuu wa Fedha** | 25/09/2023 | |
| Aloyce Leonard<br>**Mkaguzi wa Ndani** | 25/09/2023 | |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2016, na zinaonesha hali halisi.

| | Tarehe |
|---|---|
| Mussa L. Gama<br>**Mwenyekiti wa Bodi** | 25/09/2023 |
| Mohamed N. Mwinguku<br>**Mjumbe wa Bodi** | 25/09/2023 |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA - 30 SEPTEMBA, 2023

(Kiasi kwa shilingi Maelfu)

| | | Robo Mwaka ya Sasa 30/09/2023 | Robo Mwaka Iliyopita 30/09/2023 | Mwaka wa Sasa 30/09/2023 | Mwaka Uliopita 30/09/2022 |
|---|---|---|---|---|---|
| I: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/ (Hasara) Halisi | 47,146 | (25,096) | (11,172) | 68,968 |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara katika Mali | (15,845) | 19,895 | 16,659 | 33,756 |
| | - Badiliko halisi katika Mikopo | (293,061) | (136,790) | (696,272) | 138,671 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi katika Amana | (189,383) | 330,379 | (302,159) | (477,560) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 147,522 | 14,927 | 194,063 | (110,890) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (50,755) | 22,981 | (41,986) | 193,065 |
| | - Kodi iliyolipwa | - | 3,000 | 6,000 | 40,680 |
| | - Mengineyo (bainisha) | (26,129) | 62,132 | (17,099) | (186,026) |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(380,505)** | **291,428** | **(851,966)** | **(299,336)** |
| II: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji** | | | | |
| | Gawio Lilopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - | (90,836) | (28,538) | 131,364 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| | Ununzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Uwekezaji** | **-** | **(90,836)** | **(28,538)** | **131,364** |
| III: | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| | Gawio Lilolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 297,813 | - | 797,813 | - |
| | Mengineyo ( bainisha) | - | - | - | - |
| | **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **297,813** | **-** | **797,813** | **-** |
| IV: | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (82,692) | 200,592 | (82,692) | (167,972) |
| | Fedha Taslimu na Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 843,476 | 642,884 | 843,476 | 553,051 |
| | **Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka/Mwaka** | **760,784** | **843,476** | **760,784** | **385,080** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA - 30 SEPTEMBA, 2023 Mwaka wa sasa

(Kiasi kwa Shilingi maelfu)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa Sasa-30/06/2023** | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 4,483,228 | - | (2,339,556) | 173 | - | 153,306 | **2,297,150** |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (11,172) | - | - | - | **(11,172)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | **(17,665)** | **17,665** | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | **(35,679)** | **(35,679)** |
| Mengineyo | - | - | **9,124** | - | - | - | **9,124** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **4,483,228** | **-** | **(2,359,269)** | **17,838** | **-** | **117,627** | **2,259,423** |
| **Mwaka uliopita-31/12/2022** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **4,483,228** | - | **(2,392,795)** | **74,225** | - | **87,456** | **2,252,113** |
| Faida/(Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (20,813) | - | - | - | **(20,813)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | **74,052** | **(74,052)** | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | **65,850** | **65,850** |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **4,483,228** | **-** | **(2,339,556)** | **173** | **-** | **153,306** | **2,297,150** |

### TANDAHIMBA COMMUNITY BANK PLC
## MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES

| Sn | BANK CHARGES 2023<br>Transactions | Description | Previous Rates 2023<br>VAT Exclusive | Previous Rates 2023<br>VAT Inclusive | New Rates 2023<br>VAT Exclusive | New Rates 2023<br>VAT Inclusive |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Account Maintenance Fee** | | | | | |
| | Individual Savings | Per Month | 2,500 | 2,950 | 2,500 | 2,950 |
| | Company Savings | Per Month | 13,000 | 15,340 | 13,000 | 15,340 |
| | **Group saving** | | | | - | - |
| | Amcos Collection | Per Month | 13,000 | 15,340 | 13,000 | 15,340 |
| | Amcos Business | Per Month | Free | Free | Free | Free |
| | Local council | Per Month | 13,000 | 15,340 | 13,000 | 15,340 |
| | Group saving | Per Month | 3,500 | 4,130 | 3,500 | 4,130 |
| 2 | **Min account Opening** | | | | | |
| | Individual Savings | Per Month | 10,000 | N/a | 10,000 | N/a |
| | Company Savings | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | **Group saving** | | | | | |
| | Amcos Collection | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | Amcos Business | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | Local council | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | Group saving | Per Month | 20,000 | N/a | 20,000 | N/a |
| 3 | **Min operating Balance** | | | | | |
| | Individual Savings | Per Month | 10,000 | N/a | 10,000 | N/a |
| | Company Savings | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | **Group saving** | | | | | |
| | Amcos Collection | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | Amcos Business | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | Local council | Per Month | 50,000 | N/a | 50,000 | N/a |
| | Group saving | Per Month | 20,000 | N/a | 20,000 | N/a |
| 4 | **Cash withdral Over the counter** | | | | | |
| | From TZS 1,000-4,999 | Per transaction | 300 | 354 | 300 | 354 |
| | From TZS 5,000-9,999 | Per transaction | 750 | 885 | 750 | 885 |
| | From TZS 10,000-19,999 | Per transaction | 1,200 | 1,416 | 1,200 | 1,416 |
| | From TZS 20,000-39,999 | Per transaction | 1,650 | 1,947 | 1,650 | 1,947 |
| | From TZS 40,000-49,999 | Per transaction | 2,000 | 2,360 | 2,000 | 2,360 |
| | From TZS 50,000-99,999 | Per transaction | 3,500 | 4,130 | 3,500 | 4,130 |
| | From TZS 100,000-199,999 | Per transaction | 4,500 | 5,310 | 4,500 | 5,310 |
| | From TZS 200,000-299,999 | Per transaction | 5,500 | 6,490 | 5,500 | 6,490 |
| | From TZS 300,000-599,999 | Per transaction | 6,500 | 7,670 | 6,500 | 7,670 |
| | From TZS 600,000-799,999 | Per transaction | 7,000 | 8,260 | 7,000 | 8,260 |
| | From TZS 800,000-999,999 | Per transaction | 7,500 | 8,850 | 7,500 | 8,850 |
| | From TZS 1,000,000-2,999,999 | Per transaction | 8,000 | 9,440 | 8,000 | 9,440 |
| | From TZS 3,000,000-4,999,999 | | 9,500 | 11,210 | 9,500 | 11,210 |
| | 5,000,000 - Above | | 9,500+0.12% of excess max 170,000 | 9,500+0.12% of excess max 170,000 | 9,500+0.12% of excess max 170,000 | 9,500+0.12% of excess max 170,000 |
| | Mwana A/C cash withdrawal exceeding 3rd transaction per annum | Per transaction | 3,000 | 3,540 | 3,000 | 3,540 |
| 5 | **Cash withdral - TACOBA Agency Banking** | | | | | |
| | From TZS 0-499 | Per transaction | N/a | N/a | 250 | 295 |
| | From TZS 500-999 | Per transaction | N/a | N/a | 250 | 295 |
| | From TZS 1,000-1,999 | Per transaction | N/a | N/a | 250 | 295 |
| | From TZS 2,000-2,999 | Per transaction | N/a | N/a | 300 | 354 |
| | From TZS 3,000-3,999 | Per transaction | N/a | N/a | 300 | 354 |
| | From TZS 4,000-4,999 | Per transaction | N/a | N/a | 300 | 354 |
| | From TZS 5,000-6,999 | Per transaction | N/a | N/a | 700 | 826 |
| | From TZS 7,000-9,999 | Per transaction | N/a | N/a | 700 | 826 |
| | From TZS 10,000-14,999 | Per transaction | N/a | N/a | 1,150 | 1,357 |
| | From TZS 15,000-19,999 | Per transaction | N/a | N/a | 1,150 | 1,357 |
| | From TZS 20,000-29,999 | Per transaction | N/a | N/a | 1,500 | 1,770 |
| | From TZS 30,000-39,999 | Per transaction | N/a | N/a | 1,500 | 1,770 |
| | From TZS 40,000-49,999 | Per transaction | N/a | N/a | 2,000 | 2,360 |
| | From TZS 50,000-99,999 | Per transaction | N/a | N/a | 3,200 | 3,776 |
| | From TZS 100,000-199,999 | Per transaction | N/a | N/a | 3,950 | 4,661 |
| | From TZS 200,000-239,999 | Per transaction | N/a | N/a | 5,300 | 6,254 |
| | From TZS 240,000-299,999 | Per transaction | N/a | N/a | 5,300 | 6,254 |
| | From TZS 300,000-399,999 | Per transaction | N/a | N/a | 6,500 | 7,670 |
| | From TZS 400,000-499,999 | Per transaction | N/a | N/a | 6,800 | 8,024 |
| | From TZS 500,000-599,999 | Per transaction | N/a | N/a | 7,500 | 8,850 |
| | From TZS 600,000-699,999 | Per transaction | N/a | N/a | 7,700 | 9,086 |
| | From TZS 700,000-799,999 | Per transaction | N/a | N/a | 8,000 | 9,440 |
| | From TZS 800,000-899,999 | Per transaction | N/a | N/a | 8,000 | 9,440 |
| | From TZS 900,000-999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 8,500 | 10,030 |
| | From TZS 1,000,000-1,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 8,720 | 10,290 |
| | From TZS 2,000,000-2,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 8,720 | 10,290 |
| | From TZS 3,000,000-3,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 9,600 | 11,328 |
| | From TZS 4,000,000-4,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 9,600 | 11,328 |
| | From TZS 5,000,000-5,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 10,000 | 11,800 |
| | From TZS 6,000,000-6,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 11,000 | 12,980 |
| | From TZS 7,000,000-7,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 12,500 | 14,750 |
| | From TZS 8,000,000-8,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 14,000 | 16,520 |
| | From TZS 9,000,000-9,999,999 | Per transaction | N/a | N/a | 15,000 | 17,700 |
| | From TZS 10,000,000 & Above | Per transaction | N/a | N/a | 15,000 | 17,700 |
| 6 | **Activation of Dormant Accounts** | | | | | |
| | All other accounts | Free | Free | Free | Free | Free |
| | Saving account of personal loan customers | Per account | Free | Free | Free | Free |
| 7 | **Closing of Account** | | | | | |
| | Saving account | Per account | 5,000 | 5,900 | 5000 | 5900 |
| | All other accounts | Per account | 10,000 | 11,800 | 10000 | 11800 |
| 8 | **Inter-Bank (Outward Funds Transfer)** | | | | | |
| | TISS | Per transaction | 10,000 | 11,800 | 10000 | 11800 |
| | **Inter-Bank (Inward Funds Transfer)** | | | | | |
| | Internal Transfer | Per transaction | 1,000 | 1,180 | 1000 | 1180 |
| 9 | **Cards** | | | | | |
| | **New Cards** | | | | | |
| | Tacoba card | Per card | 5,000 | 5,900 | 5,000 | 5,900 |
| | Korosho card | Per card | 11,000 | 12,980 | 11,000 | 12,980 |
| | **New Cards due to expired** | | | | | |
| | Tacoba card | Per card | 5,000 | 5,900 | 5,000 | 5,900 |
| | Korosho card | Per card | 11,000 | 12,980 | 11,000 | 12,980 |
| | **Peplacement due to lost/spoiled** | | | | | |
| | Tacoba card | Per card | 10,000 | 11,800 | 10,000 | 11,800 |
| | Korosho card | Per card | 22,000 | 25,960 | 22,000 | 25,960 |
| | Annual card fee All Cards | per card | 10,000 | 11,800 | 10,000 | 11,800 |
| 10 | **Account statements** | | | | | |
| | Interim statement per month | per transaction | Free | Free | Free | Free |
| | Quartely statement | per transaction | 2,500 | 2,950 | 3,000 | 3,540.00 |
| | Adhoc from 4 up to 12 month | per transaction | 10,000 | 11,800 | 15,000 | 17,700.00 |
| | Adhoc above 12 month | per transaction | 20,000 | 23,600 | 20,000 | 23,600 |
| 11 | **Salary and Bulk payment** | | | | | |
| | Salary and Bulk payment fee | per transaction | 4,500 | 5,310 | 5,000 | 900 |
| | Transfer to other Banks | per transaction | 5,000 | 5,900 | 3,000 | 540 |
| | Balance enquiry | per request | 500 | 590 | Free | Free |
| 12 | **Information search** | | | | | |
| | For information up to 12 past months | per document | 50,000 | 59,000 | 50,000 | 59,000 |
| | For information of 1 to 5 past years | per document | 80,000 | 94,400 | 80,000 | 94,400 |
| | For information above 5 years | per document | 100,000 | 118,000 | 100,000 | 118,000 |
| | CCTV Image retrieve | Per request | 100,000 | 118,000 | 100,000 | 118,000 |
| 13 | **Introduction Letter and certificate of Balance** | | | | | |
| | Cerfificate of balance | per item | 50,000 | 59,000 | 50,000 | 59,000 |
| | status report | per report | 50,000 | 59,000 | 50,000 | 59,000 |
| | Visa recommendation | per item | 50,000 | 59,000 | 50,000 | 59,000 |
| | Any other introduction | per item | 50,000 | 59,000 | 50,000 | 59,000 |
| | Bank statement requested by other banks | per item | 50,000 | 59,000 | 50,000 | 59,000 |
| 14 | **Loan Fees** | | | | | |
| 1 | **MSE** | | | | | |
| | Loan Application fee | | 1% | | 1% | |
| | Facility Fee | | 1% | | 1% | |
| | Legal documentation fee | | 0.5% | | 1% | |
| 2 | **AGRICULTURE LOANS** | | | | | |
| | Loan fee | 0-999,999 | 100,000 | 118,000 | 100,000 | 118,000 |
| | Loan fee | 1mn - 1,999,999 | 200,000 | 236,000 | 200,000 | 236,000 |
| | Loan Application fee | 2mn and above | 1% on Loan amount | | 1% on Loan amount | |
| | Facility Fee | | 2% on Loan amount | | 2% on Loan amount | |
| | Legal documentation fee | | 1% on Loan amount | | 1% on Loan amount | |
| 3 | **PERSONAL LOAN** | | | - | | |
| | Loan Application fee | | 0.55% MIN 55,000 | | 0.55% MIN 55,000 | |
| | Facility Fee | | 1% MIN 90,000 | | 1% MIN 90,000 | |
| | Legal documentation fee | | Free | | Free | |
| 4 | **GROUP LOAN** | | | | | |
| | Loan Application fee | | 1% on Loan amount | | 1% on Loan amount | |
| | Facility Fee | | 2% on Loan amount | | 2% on Loan amount | |
| | Legal documentation fee | | 1% on Loan amount | | 1% on Loan amount | |
| 5 | **ASSET FINANCING LOAN** | | | | | |
| | Loan Application fee | | 1% on Loan amount | | 1% on Loan amount | |
| | Facility Fee | | 1% on Loan amount | | 1% on Loan amount | |
| | Legal documentation fee | | 0.5% on Loan amount | | 0.5% on Loan amount | |
| 6 | **CHAPCHAP LOAN** | | | | | |
| | Loan Application fee | | Free | | Free | |
| | Facility Fee | | | 3% Min 59,000 VAT INCL | 0% | |
| | Legal documentation fee | | Free | | Free | |
| 15 | **charges on early loan payment** | | | | | |
| | Salary loan | | 5.9% min 500,000 | | 5.9% min 500,000 | |
| | MSE business loan | | 3% on the unpaid amount min 500,000 | | 3% on the unpaid amount min 500,000 | |
| | Agriculture loan | | Free | | Free | |
| | Other segment | | 3% on the unpaid amount | | 3% on the unpaid amount | |
| | Restructuring Fee | | 2% min 150,000 | 177,000 | 2% min 150,000 | 177,000 |
| 16 | **Cheque Book order** | | | | | |
| | Per leaf - 100 | | 1,000 | 1,180 | 1,000 | 1,180.00 |



## Zahanati yajengwa kwa miaka 10, wananchi wanililia serikali

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

WANANCHI wa Kijiji cha Nyasingu Kata ya Igalula Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza, wameomba serikali kusaidia kukamilisha ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho, ambayo wamekuwa wakiijenga kupitia michango yao kwa zaidi ya miaka 10 bila kukamilika.

Inaelezwa kuwa adha ya wananchi hao kutembea umbali wa zaidi ya kilometa sita kufuata huduma za afya katika zahanati za vijiji jirani vya Lubungo na Sotta iliwalazimu kuanza kuchangia fedha za kujenga zahanati yao, lakini mpaka sasa ni zaidi ya miaka 10 bado haijakamilika.

Wanakijiji hao walitoa ombi hilo mbele ya Kamati ya Siasa ya Wilaya ya Sengerema iliyofika katika vijiji hivyo kwa ajili ya kuzungumza na kusikiliza kero zao na kueleza namna wanavyosumbuka kupata huduma za afya.

"Huduma tunazipata kwa shida na hali hii ndiyo ilitufanya kujenga zahanati yetu ambayo tumekuwa tukichangia ujenzi wake zaidi ya miaka 10 sasa lakini haikamiliki, tunaomba serikali isaidie kuikamilisha na sisi tupate huduma karibu yetu," alisema mmoja wa wananchi hao Hamis Juma.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Sengerema, Marck Augustine Makoye alitoa ombi lake kwa Mkurugezi Mtendaji wa Halmashauri hiyo kutumia mapato ya ndani ili waweze kuwasaidia wananchi wa kijiji hicho kukamilisha ujenzi wa zahanati yao.

Diwani wa Kata ya Igalula, Phaustine Shibiliti alisema tayari ameshaiombea zahanati hiyo bajeti ya Sh.milioni 50 kwa ajili ya ukamilishwaji wake, hali itakayowasaidia wananchi kuondokana na tatizo la kukosa huduma za afya kijijini hapo.

# Waliodaiwa kulipwa kufanya mauaji waachiwa huru kortini

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Rufani Kanda ya Mwanza imewafutia hatia na adhabu ya kifo Petro Sure na wenzake watatu baada ya kubaini polisi hawakuzingatia haki za warufani wakati wanachukua maelezo ya onyo.

Hukumu hiyo ya mahakama ilitolewa jana mbele ya jopo la majaji watatu; Jaji Shaaban Lila, Jaji Patricia Fikirini na Jaji Zainab Muruke. Mahakama iliamuru warufani Petro, Sulyu Jinasa, Mwandu Hotel na Bode Hamisi waachiwe huru baada ya kuikubali rufani waliyowasilisha wakipinga kutiwa hatiani na adhabu ya kifo iliyotolewa na Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza.

Inadaiwa kuwa Novemba 5, 2012, katika Kijiji cha Shirima wilayani Kwimba, mkoani Mwanza, warufani kwa pamoja walimuua Kulwa Makalwe.

Warufani walipinga hukumu hiyo wakiwa na sababu saba ikiwamo maelezo ya onyo yalichukuliwa kimakosa na walitiwa hatiani kwa kuzingatia maelezo ya onyo yaliyochukuliwa kimakosa kwa kutumia vifungu mbalimbali vya sheria.

Katika kesi hiyo, upande wa mashtaka uliita mashahidi wanane kwa nia ya kuthibitisha kosa. Kulingana na shahidi wa kwanza ambaye alikuwa na wake wawili akiwamo marehemu, tukio hilo lilitokea Novemba 5 mwaka 2012 saa 1:30 usiku.

Alidai watu wawili walikwenda nyumbani kwake na kumkuta amekaa nje na marehemu wakisubiri chakula cha jioni, Kwa msaada wa mbalamwezi, alifanikiwa kuwaona na kuwatambua kuwa warufani wa pili na wa tatu ambao hawakuwa wageni kwake. Waliishi kijiji kimoja.

Alidai wa kwanza alishika panga ambalo alimkata marehemu na alikuwa amevaa koti jeusi na kofia nyeusi na mwingine alikuwa amevaa shati la rangi ya kijani la mikono mirefu. Shahidi huyo ambaye ni mume wa marehemu alidai baada ya mashambulizi alikimbia kwa jirani yake, Mussa Chenya ambaye ni shahidi wa pili. Alimtajia majina ya warufani wawili ndio waliowavamia.

Iliadaiwa waliporudi kwenye eneo la uhalifu, walimkuta Makalwe amepoteza fahamu, walimpeleka hospitalini, lakini alifariki dunia muda mfupi baadaye. Shahidi huyo aliripoti tukio hilo polisi Novemba 11, 2012 na kurekodi maelezo yake.

Aliendelea kudai kwamba baada ya wiki moja, warufani hao wawili walimwita kwenye eneo la mnada na kumwambia asiwalaumu kwa kumuua mkewe kwa sababu wameajiriwa kufanya tukio hilo, mrufani wa kwanza anamtuhumu mkewe kuwa ni mchawi na wakamwonya asiwafichue, la sivyo wangemuua.

Baada ya kupitia ushahidi na kusikiliza hoja za mawakili wapande zote mbili, jopo lilisema linakubaliana na Wakili wa Jamhuri Morice Mtoi kwamba mtuhumiwa hana la kufanya ili kutimiza matakwa ya kifungu cha 57(4) cha CPA.

Wakili huyo anadai maofisa wa polisi waliorekodi taarifa hawakutekeleza wajibu wao wa kisheria kama ilivyoainishwa.

Alidai wanaacha kumbukumbu izungumze yote kwa kunukuu aya mbili za mwisho wa taarifa ya kila mrufani iliyoonya.

Jopo lilisema sehemu zilizonukuliwa kwenye maelezo ya onyo ya warufani ni wazi kuwa taarifa zote ziliandikwa na polisi kulingana na ushahidi kwenye kumbukumbu.

Haki za watuhumiwa hazikuzingatiwa na taarifa ya mrufani wanne ambayo inaonesha kiwango chake cha elimu kuwa darasa la saba.

Mahakama inasema kifungu cha 53 cha CPA kinaeleza haki za mshtakiwa zinapaswa kujulikana kabla ya kuhukumiwa, kuuliza au kuulizwa kufanya chochote kama kuandika taarifa.

"Ni wajibu wa ofisa wa polisi akimhoji mtu kwanza hakikisha kutoka kwake kama anajua kusoma na kuandika na hajui anataka kuandika taarifa mwenyewe kabla ya kufanya kitu chochote.

"Kwa bahati mbaya, hii haikufanywa kwa kuwa hakuna maneno kama hayo katika kumbukumbu, maofisa polisi walirekodi taarifa bila kuzingatia majukumu yao na haki za warufani.

"Kwa kuwa, masharti haya yote ni ya lazima, ukiukaji wao ni mbaya, hatuna uamuzi mwingine ila kufuta taarifa zote za warufani kama tunavyofanya.

"Kwa kuzingatia kwamba ushahidi wa kuona wa shahidi wa kwanza hautoshi na kwa kufuta taarifa zote zilizoonywa, hakuna ushahidi mwingine ambao hukumu za warufani zinaweza kuzingatiwa. "Tunaruhusu rufani, tunafuta hukumu na adhabu, tunaamuru warufani wote waachiwe huru isipokuwa kama kuna sababu nyingine halali za kuwaweka gerezani, " lilisema jopo.



Meneja Miradi kutoka Shirika la Msaada wa Kisheria mkoani Shinyanga (PACESH), John Shinja (kulia), akitoa elimu ya sheria ya ndoa na kupinga vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo kuacha kuozesha wanafunzi, ndoa za utotoni na kuwapatia ujauzito kwa wananchi wa kijiji cha Wishiteleja, wilayani Kishapu juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Ukerewe yapewa kipaumbele mgawo wa walimu

**Na Vitus Audax,** UKEREWE

MKUU wa Wilaya ya Ukerewe, Hassan Bomboko amesema serikali imeendelea kutoa kipaumbele katika mgawo wa walimu visiwani hapa.

Visiwa hivyo ni pamoja na Irugwa, Ukara, Bwiro na Kwiru ambavyo vimepangiwa walimu kwa miaka miwili mfululizo kuanzia mwaka 2021 hadi 2022 pamoja na ujenzi wa madarasa na shule mpya kupitia miradi ya Boost, Ep4r, Swash, GPE pamoja na TEA.

Bomboko alitoa taarifa hiyo wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake na kueleza kuwa maeneo hayo ya visiwani hapa awali yalikuwa yakikimbiwa na walimu kutokana na kutokuwa na miundombinu.

"Mwalimu alikuwa akipangwa Ukerewe ilikuwa wanakaa miezi sita hadi mwaka kisha wanaomba kuhamishwa au kubadilishana. Lakini kwa sasa maeneo haya ya visiwa tumeyafanya kuwa ya kimkakati kwa kuhakikisha huduma zote za kielimu zinawafikia," alisema.

Aidha, aliongeza kuwa kwa sasa wanaendelea kuiomba Wizara ya Elimu kuendelea kuiangalia Ukerewe kwa jicho la ziada kama kanda maalumu katika sekta ya elimu kulingana na asili yake ya kuwa na visiwa vingi ili iendelee kukua kielimu.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mlezi iliyopo Kata ya Bukanda, Simeo Charles alisema wameendelea kuboreshewa miundombinu pamoja na kuongezewa walimu ili kusaidia katika ufundishaji na malezi ya wanafunzi.

Aidha, alisema shule hiyo imejengewa madarasa manne pamoja na vyoo hali ambayo imetatua adha ya wanafunzi kulundikana darasani na ukosefu wa vyoo.

"Tunahitaji pia kuongezewa nyumba za walimu kwani kwa sasa tunazo mbili tu, huku walimu katika shule hii tukiwa 10, hivyo kulazimu walimu wengine kutafuta sehemu za kupanga," alisema.

Baadhi ya wanafunzi katika shule hiyo walieleza namna walivyokuwa wakipata adha katika masomo yao kufuatia shule hiyo kuwa na miundombinu mibovu ya kusomea.





# MSD yatakiwa kuongeza kasi usambazaji vifaa tiba

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imeiagiza Bohari ya Dawa (MSD) kusambaza kwa wakati vifaa tiba kwenye vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya mkoani hapa, ambavyo vimelipiwa ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Afya ya Msingi ya Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa agizo hilo juzi wakati akifungua kikao cha kamati hiyo kilichokuwa na lengo la kufanya tathimini ya upatikanaji wa huduma mbalimbali za afya ikiwemo chanjo na miundombinu.

Homera ambaye pia ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, alisema MSD wamekuwa wakichelewa kusambaza vifaa hivyo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya hata kama wamelipwa, hali ambayo inasababisha huduma kwa wananchi kukwama.

**Miundombinu yote iliyopelekewa fedha inatakiwa kukamilika ndani ya miezi mitatu ili shughuli zingine za maendeleo ziendelee kufanyika.**

Alisema, kwa sasa mkoa huo umepokea zaidi ya Sh. bilioni 2.4 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba na hivyo akawataka watendaji wa bohari hiyo kuhakikisha wanasambaza vifaa hivyo kwa wakati kwenye maeneo yote.

"Sasa nawapa salaam ninyi MSD, kwa hizi fedha ambazo tumepokea sasa hivi hakikisheni mnasambaza vifaa hivi kwa wakati, mmekuwa mkichelewesha sana, mtu anaomba vifaa sasa hivi mnaleta mwakani," alisema Homera.

Vilevile aliwataka wafanyakazi wa idara ya afya katika mkoa huo kuhakikisha wanafanya kazi vizuri na kwa kuzingatia miiko ya kazi yao ili kuwasaidia wananchi ambao wanakwenda kupata huduma kwenye maeneo hayo.

Alisisitiza pia wasimamizi wa vituo vya afya kwenye mkoa huo kuhakikisha wanasimamia ujenzi wa miundombinu mbalimbali ambayo imeletewa fedha ili ianze kutumika.

Alisema miundombinu yote iliyopelekewa fedha inatakiwa kukamilika ndani ya miezi mitatu ili shughuli zingine za maendeleo ziendelee kufanyika.

Ofisa Uelimishaji na Uhamasishaji wa Wizara ya Afya, Penford Joel alisema serikali imewekeza nguvu na fedha nyingi kwenye uimarishaji wa huduma za afya kutokana na kwamba ni sekta muhimu na nyeti.

Alisema huduma za matibabu ni gharama kubwa na hivyo ili wananchi waepukane nazo wanatakiwa kuwekeza nguvu kwenye kujikinga na magonjwa pamoja na kuwakinga wengine.

Alisema Wizara ya Afya itaendelea kusimamia ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo inayohusiana na sekta hiyo ili kuwasogezea wananchi huduma.



Mkuu wa wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo akizungumza na wananchi wakati wa ziara yake ya "ulipo nipo toa kero yako sema kweli sio majungu" katika kata ya Ruponda na kata ya Chiola juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Ndalichako akemea matumizi ya kuni, mkaa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Dk.Joyce Ndalichako amekemea matumizi ya kuni na mkaa akisema yamekuwa na athari kubwa za kiafya.

Hivyo, ameshauri wananchi wakatumia nishati safi ya kupikia ili kuhakikisha afya za wananchi zinakuwa salama.

Aliyasema hayo wakati wa ugawaji wa mitungi ya gesi 600 kutoka kampuni ya Oryx 600 pamoja na majiko kwa wanawake wa makundi mbalimbali ya Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma.

Waziri Ndalichako ambaye pia ni Mbunge wa Kasulu Mjini amesema mitungi hiyo inakwenda kuleta auheni kwa makundi ya wanawake kwani wataachana na matumizi ya kuni na mkaa na kutumia nishati safi ya kupikia ambayo ni gesi ya oryx.

Alisema matumizi ya kuni na mkaa yamekuwa na athari kubwa za kiafya hivyo ni vema wananchi wakatumia nishati safi ya kupikia ili kuhakikisha afya za wananchi zinakuwa salama.

Akizungumza wakati wa ugawaji wa mitungi hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Oryx Gas Tanzania, Araman Bonoite alisema mipango yao ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia inakwenda na mpango wa Serikali wa miaka 10 wa matumizi salama ya nishati safi ya kupikia.

Alisema: "Tunafahamu kuwa kundi hili la kinamama ambao kila siku wanahudumia chakula cha Watanzania wengi, wameathirika kutokana na matumizi ya kuni na mkaa hivyo, kampuni ya Oryx Gas kwa kushirikiana na Waziri Ndalichako wameamua kuiunga mkono jumuiya hii ikiwa ni hamasa kwa wengine".

Alisema Mkoa wa Kigoma na mikoa jirani imeharibiwa kwa kiasi kikubwa na ukataji miti kwa ajili ya matumizi ya nishati ya kupikia chakula, hivyo jitihada kubwa zinahitajika ili kulinda afya na kuokoa mazingira ya mkoa.

Benoite alisema Rais Samia ameweka lengo la Watanzania kutumia nishati safi, ikiwa ni pamoja na LPG, kuwa angalau asilimia 80 ya Watanzania ifikapo mwaka 2032.

## FCC kuendeleza msako ukamataji bidhaa bandia

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

TUME ya Ushindani (FCC) Nyanda za Juu Kusini imesema itaendelea kutoa elimu kwa wajasiriamali na wananchi juu ya kutambua bidhaa bandia ili kudhibiti zisiingie sokoni.

Mkuu wa Kanda FCC Nyanda za Juu Kusini, Dickson Mbanga, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari mkoani hapa wakati wa maonesho ya viwanda vidogo kitaifa.

Mbanga alisema wafanyabiashara na wazalishaji wanaowajibu wa kusajili nembo zao ili kulindwa na sheria ya alama za bidhaa zao dhidi ya wazalishaji wanaoiga bidhaa zao kwa nia ya kudanganya au kutapeli.

Alisema, wazalishaji au wajasiriamali wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanaonyesha taarifa zote muhimu katika vifungashio kama Sheria ya Alama za Bidhaa ya Mwaka 1963 ilivyoelekeza.

Alisema sheria imeweka wazi kuwa atakayekutwa na bidhaa bandia kwanza anatakiwa kulipa faini ya fedha kulingana na thamani ya bidhaa husika kisha bidhaa hiyo inateketezwa kwa moto.

## Wapongeza Lishe kwa vijana

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wilayani Chunya mkoani Mbeya, wamepongeza hatua ya serikali kuanzisha kampeni ya lishe kwa vijana balehe.

Wamesema serikali imechukua hatua nzuri kuwa na mpango wa kutoa elimu ya lishe kwa vijana balehe wakiwemo wanafunzi wa shule za sekondari kwa maelezo kuwa itawawezesha kuimarisha afya zao na jamii inayowazunguka.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa wananchi hao, Dionese Mamboleo mkazi wa Kijiji cha Nkwangu Kata ya Upendo, alisema wanaiona kampeni hiyo kuwa na umuhimu zaidi kwa vijana.

Mamboleo alisema vijana balehe wakitambua lishe bora watakuja kuwa walezi bora wa familia zao kwa kuzingatia mambo muhimu ikiwemo namna wajawazito na watoto wachanga wanavyopaswa kulishwa ili kuwawezesha kuwa na afya imara.

Mkazi wa Makongolosi, Tumaini Nelson alisema kampeni ya lishe kwa vijana balehe inawajengea msingi vijana kuja kuwa mama na baba bora kwa familia zao watakapoingia kwenye ndoa na watazingatia kanuni za kuondokana na udumavu.





# Dk. Mwinyi atoa angalizo ongezeko la watu duniani

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema ongezeko la watu duniani linachangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa mahitaji muhimu ya kibinadamu ikiwemo maji.

Alisema tatizo hilo pia husababisha uhaba wa huduma na vifaa mijini na vijijini na kuchangia chachu ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi.

Aliyasema hayo jana visiwani hapa wakati akifungua Kongamano la 24 la Maji, lililoyashirikisha mataifa kutoka Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Alisema hali hiyo huibua masuala mbalimbali ikiwamo kuzorota kwa vyanzo vya maji, uchafuzi wa mazingira, upotevu wa viumbe hai na upotevu wa afya ya mazingira kwa ujumla.

Rais Dk. Mwinyi alisema changamoto hizo zinahitaji usimamizi endelevu wa rasilimali za maji ili kukidhi mahitaji ya sasa ya kiikolojia, kijamii na kiuchumi bila kuathiri uwezo wa kukidhi mahitaji hayo kwa siku zijazo.

Alisema kongamano hilo limekuja wakati mwafaka wakati mataifa ya Kusini mwa Afrika yakiendeleza mchakato wa kuharakisha mabadiliko kupitia mbinu za kiubunifu na utengamano kwa ajili ya usimamizi endelevu wa rasilimali za maji kwenye mataifa yao.

Aidha, alisema Zanzibar ilianzisha mpango wa uwekezaji maji wa mwaka 2022 hadi 2027 uliolenga kukusanya rasilimali kwa ajili ya uwekezaji wa usalama wa maji.

Dk. Mwinyi alisema mpango huo umezingatia maeneo matano yakiwemo uwekezaji wa maji na fedha kwa ajili ya kuboresha huduma za maji na usafi wa mazingira, kujenga uwezo wa kuhimili hali ya hewa, usawa wa kijinsia na ushirikishwaji wa kijamii, kuimarisha utaratibu wa kitaasisi, pamoja na uchumi wa buluu na usimamizi endelevu wa rasilimali maji.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Omar Juma Kipanga, alipongeza juhudi zinazochukuiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kukuza sekta ya maji kupitia uchumi wa buluu.

Naibu Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Zanzibar, Shaaban Ali Othman alisema jitihada kubwa zinaendelea kuchukuliwa na Serikali ya Zanzibar katika kuwaondolea changamoto ya maji wananchi, kuhakikisha usalama wa maji safi unaendelea kupatikana maeneo yote ya Zanzibar.

Mtaalamu wa mazingira kutoka Namibia, Profesa. Nnenesi Kgabi, alisema mkutano huo ni fursa muhimu ya kubadilishana uzoefu na ushirikiano baina ya washiriki ambao unadumisha uhusiano uliopo baina ya mataifa ya kusini mwa bara la Afrika.

# Serikali yataja faida za kiuchumi uanzishaji kituo cha teknolojia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema kuwa uamuzi wa kampuni ya Air Pay kuanzisha kituo cha teknolojia nchini kutachochea kasi ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania.

Aliyasema hayo wakati akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa kampuni hiyo, ulioenda sambamba na uzinduzi wa Mtandao wa Idara ya Ushirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi (PPP).

Alisema mfumo huo utakuza uchumi wa nchi hasa ikizingatiwa kuwa Serikali ya Zanzibar inatekeleza sera za uchumi wa buluu na inajitahidi kuweka mazingira mazuri ili kuvutia wawekezaji.

Akizungumzia ajenda ya mifumo ya digitali nchini, alitoa rai kwa taasisi mbalimbali za serikali kutumia mifumo ya wakala wa serikali mtandao na kuitaka taasisi hiyo kuhakikisha usalama wa mifumo inayoanzishwa ili kupunguza changamoto za kifedha.

Aidha, aliishauri kuzisaidia taasisi na mashirika ya umma kuyafikia masoko ya kidijitali ili kutatua changamoto mbalimbali ikiwemo kujenga utamaduni wa matumizi ya mifumo ya malipo kidijitali badala ya fedha taslimu.

Alisema kwa kipindi kirefu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imekua ikijaribu kutafuta suluhisho kutoka katika matumizi ya fedha taslimu na kwenda kulipia kimtandao ambao hakuna sababu ya kubeba fedha kwa ajili ya kununua bidhaa au kufanya malipo mbalimbali.

Alisema pia ni fursa kwa wajasiriamali kutambulika na kuweza kupata mikopo katika taasisi mbalimbali za kifedha.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga alisema kuwa mfumo wa malipo uliozinduliwa utachangia ukuaji wa uchumi na kurahisisha ukusanyaji wa mapato ya serikali.

Alieleza kuwa mfumo huo unajumuisha makundi yote yanayohusika na biashara, ujasiriamali na uhaulishaji wa fedha na mfumo huo sio mgeni na nchi mbalimbali zinaunatumia na lengo mahsusi serikali kuwa na takwimu halisi ya mwenendo wa uchumi.

Waziri wa Biashara na Viwanda, Omar Said Shabani, alisema mfumo huo wa air pay utawezesha mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara katika kufanya malipo lakini siyo kwa wafanyabiashara pekee hata watoa huduma.

Alisema mfumo huo utaleta mapinduzi makubwa katika mazingira mazuri ya biashara, ufanyaji wa malipo na mambo mingine na wizara yake inatarajia kufanya maonesho ya kibiashara hivyo mfumo huo utumike katika ulipaji ambapo huduma hiyo ni salama.

Kamishna wa PPP, Dk. Bili Kiwia, alisema mfumo huo wa air pay utasaidia kurasimisha wajasiriamali sekta isiyo rasmi kufanya biashara kidijitali pasipo na uhitaji wa fedha taslimu.

Mwazilishi Mweza wa Air Pay Tanzania Bara, Yasmin Chali, alisema wameamua kuwekeza Zanzibar kutokana na umahiri wake kwenye biashara na uvumbuzi wa masuala mbali mbali, hivyo watajitahidi kuhakikisha uwekezaji wao unawanufaisha watu wote.



Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah (kushoto) akimnadi mgombea uwakilishi wa jimbo la Mtambwe, Hamad Khamis Hamad wakati wa kufunga kampeni za chama hicho, huko Kisiwani Pemba juzi. Uchaguzi mdogo wa jimbo hilo, utafanyika kesho Jumamosi Oktoba 28. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yafunga kampeni kwa kishindo Mtambwe

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MJUMBE wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Hemed Suleiman Abdulla amewataka wananchi wa Mtambwe kumchagua mgombea wa CCM katika uchaguzi mdogo unaotarajiwa kufanyika kesho.

Aliyasema hayo wakati akimnadi mgombea wa CCM katika jimbo hilo, Hamad Khamis Hamad wakati wa ufungaji wa kampeni za chama hicho.

Hemed alisema ongezeko la idadi ya wanachama wanaojiunga na CCM kutokea vyama pinzani ni dhahiri kuwa sera na utekelezaji wa Ilani ya CCM vimekubalika katika eneo la Mtambwe.

Alisema hivyo wananchi wanayo kila sababu ya kumchagua mgombea wa CCM ili akashirikiane na viongozi wenzake katika kuwaletea maendeleo wananchi.

Hemed alisema kuwa maendeleo yanayoletwa na serikali kupitia CCM yanawanufaisha wanachi wote, akisema kwamba wananchi wanapaswa kuondoa tofauti zao za kisiasa na kuungana pamoja katika kumchagua mgombea wa CCM.

Pia, aliwataka wanachama wapya na wale wa zamani kushirikiana katika kumuombea kura mgombea wa CCM na kuhakikisha anashinda katika uchaguzi huo mdogo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



NURU JOSEPH SAMILA anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.4033/0040 kilichotolewa Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MKWAWA SEKONDARI mwaka 2015. Cheti cha chuo chenye namba S.4033/0040 kilichotolewa na RUNGEMBA CDTI mwaka 2021. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/URA/235138/2023.

## KUPOTEA KWA VYETI



**JOVAN MUGIZI JOSTON** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S3491/0079** kilichotolewa na **BUKOBA LUTHERAN SEKONDARY SCHOOL** mwaka 2020. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0109/0914** kilichotolewa na **IHUNGO BOYS HIGH SCHOOL** mwaka 2023. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/31106/2023 na PHQ/DAR/KIN/31109/2023.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI 321 LA 2021**
**PAUL ZAKARIA.........MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**DOROTH MASSAWE......MDAIWA/WADAIWA**
**WITO KUITWA SHAURINI**
**DOROTH MASSAWE**

**POPOTE ULIPO/MLIPO**

**PAUL ZAKARIA** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 31/10/2023 saa 03:00 Asubuhi mbele ya Mh J.W.SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo

tarehe 26 mwezi 10/2023




## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**NDG.DANIEL OTMAR MBANGALA**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki kama ifuatavyo:
Blue Kadi Namba: MC 599 CGC
Aina ya Pikipiki: HAOJUE, CC 125 Chasis Namba: LC6PCJK24K0016131
Rangi ya Pikipiki: Nyekundu
Kwa yeyote atakayeiona anaombwa aripoti kwenye kituo chochote kilicho karibu.
RIPOTI YA POLISI
**PHQ/MBE/MBE/4445/2023**

## KUPOTELEWA NA VYETI



**NDG.REBEKA JULIAS MLIGO** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha IV-Nne, chenye Index na.S.1157/0057,mwaka 2022 katika shule ya sekondari Iwawa-Makete, Njombe. (Ripoti ya Polisi-PHQ/MBE/MBE/1163/2023) Pia amepotelewa na cheti cha darasa la saba,mwaka 2018 katika shule ya msingi Iwawa-Makete,Njombe.

(Ripoti ya Polisi-PHQ/MBE/MBE/1161/2023).Vyote vilitolewa na baraza la mitihani Taifa.

Kwa yeyote atakayeviona anaombwa aripoti kwenye kituo chochote cha polisi kilicho karibu. AU APIGE SIMU NAMBA: 0745-075 886 RIPOTI YA POLISI:ZIPO KWENYE MABANO

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

WU ZHOU INVESTMENT COMPANY LIMITED wanatangaza kupotelewa na kadi mbili za pikipiki aina ya HAOJUE ya kwanza yenye namba za usajili MC726CWT na yapili yenye namba za usajili MC884DBH. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya polisi: PHQ/DOD/DOD/5273/2023.
Taarifa ya polisi: PHQ/DOD/DOD/5274/2023.

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ESTHER SADOCK MALEMBO** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya BOXER 125, yenye usajili namba MC 267 CZF, CHASSIS NAMBA: MD2B15BX3MWC98136 na ENGINE NAMBA: JVXWMC43091. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/PWA/KIB/229/2023**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**CHRISTOPHER GIBSON MWALUSWASWA** anatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili T 685 DQK - BENZ, T 445 CZQ - PRADO, T 915 DCZ - RAUM. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DAR/ILA/30433/2023.**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Piga Simu 0677020701**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Watanzania wawili watoweka, Ufaransa yaonya uvamizi Gaza

**CAIRO, Misri**

RAIS wa Ufaransa Emmanuel Macron ametahadharisha kuhusu hatua ya Israel ya kutaka kuvamia ukanda wa Gaza kwa vikosi vya ardhini, akisema ni kosa kubwa.

Akizungumza akiwa nchini Misri, Rais Macron alisema kuwa uvamizi wa aina hiyo utasababisha maafa kwa raia wasio na hatia ambao wanatakiwa kulindwa.

Aliongeza kuwa jambo hilo endapo litafanywa litawadhuru raia na halitaihakikishia Israel usalama wake wa muda mrefu. Lakini alisisitiza kwamba nchi yake inatambua haki ya Israeli ya kujilinda.

"Kuhusiana na uingiliaji wa ardhini, ikiwa unalenga kabisa vikundi vya kigaidi, hili ni chaguo kwa Israeli, lakini ikiwa ni operesheni kubwa ambayo itahatarisha raia, basi katika hali hii nadhani litakuwa kosa kwa Israeli." alisema

Katika hatua nyingine, Rais wa Marekani, Joe Biden alisema hana imani na idadi ambayo Wapalestina wanaitoa kwa watu waliouawa katika mashambulizi ya mabomu yanayofanywa na Israel.

Kiongozi huyo alisema hayo wakati alipoulizwa kama Israel inafanya jitihada za kupunguza vifo na majeruhi ya raia katika mkutano na waandishi wa habari.

"Sina imani kwamba Wapalestina wanasema kweli kuhusu idadi ya watu waliouawa. Nina hakika watu wasio na hatia wameuawa, na ni gharama ya kuanzisha vita," alisema Biden.

"Waisraeli wanapaswa kuwa waangalifu sana ili kuhakikisha kuwa wanazingatia kuwalenga watu ambao wanaeneza vita hivi. Na ni kinyume na maslahi yao wakati hilo halifanyiki. Lakini sina imani na idadi ambayo Wapalestina wanaitumia," aliongeza.

Wizara ya afya inayosimamiwa na Hamas mjini Gaza ilisema kuwa zaidi ya watu 6,500 sasa wameuawa tangu Oktoba 7, vita hivyo vilipoanza.

Jeshi la Israel (IDF) limepinga madai ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi wa Kipalestina (UNRWA) kwamba akiba ya mafuta itaisha hivi karibuni katika ukanda wa Gaza.

"Ninavyojua, bado kuna umeme katika Ukanda wa Gaza. Na ripoti hii inatia shaka kidogo," msemaji wa IDF, Lt Kanali Jonathan Conricus alisema katika mkutano wa moja kwa moja, akirejelea ripoti ya UNRWA iliyotolewa Oktoba 16.

"Tulijibu madai ya UNRWA kuwaelekeza mahali Hamas ambayo inasimamia Ukanda wa Gaza inatoa chanzo cha mafuta, na bidhaa nyinginezo. Yote ipo ndani ya Ukanda wa Gaza," alisema.

"Kuna mafuta ya kutosha kuendesha hospitali na visima vya maji. Vipaumbele ni tofauti, Hamas wanapendelea kuwa na mafuta yote kwa ajili ya uwezo wake wa kupigana vita, na kuwaacha raia bila umeme," aliongeza.

Hospitali mjini Gaza zinakabiliwa na idadi kubwa ya wagonjwa wa dharura huku kukiwa na hofu kwamba usambazaji wa mafuta unaweza kuisha katika muda mfupi ujao, kulingana na UN.

Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani, Dk. Richard Peeperkorn, aliiambia BBC kwamba hospitali zinazosaidiwa na Umoja wa Mataifa zinaendeshwa kwa jenereta katika viwango vya chini kwa ajili ya shughuli za kuokoa maisha.

Katika hatua nyingine, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ilisema jana kuwa Watanzania wawili kati ya 260 waliokuwa kwenye mafunzo ya kilimo Israel, hawajulikani waliko.

Wizara hiyo ilibainisha katika taarifa yake kuwa serikali kwa kushirikiana na mamlaka mbalimbali za Israel, inaendelea na juhudi za kutafuta ili kuwapeleka katika mazingira salama.

"Familia za vijana hao zimejulishwa kuhusu jitihada hizo na serikali inaendelea kuwasiliana nazo. Watanzania tisa wanaoishi Israel waliitikia wito wa mpango wa serikali kuwarejesha nyumbani. Walirejeshwa Tanzania Oktoba 18 mwaka huu," ilibainisha taarifa ya wizara hiyo.

**BBC**




Waziri wa Madini wa Malawi, Monica Chang'anamuno (kushoto), akikabidhi tuzo ya mshindi wa jumla katika kipengele cha uhifadhi mazingira, afya na usalama mahala pa kazi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa GGML, Terry Strong jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Waziri wa Madini, Anthony Mavunde. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Mashine mpya Ocean Road kuanza kazi mwezi ujao

**Na Faustine Feliciane**

MKURUGENZI Mtendaji Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Dk. Julius Mwaiselage, amesema mashine mpya za matibabu ya saratani zilizonunuliwa na serikali zitaanza kufanya kazi mwezi ujao.

Akipokea misaada mbalimbali kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (GBT) hospitalini huko juzi, Dk. Mwaiselage alisema kazi ya kusimika mashine hizo imekamilika na sasa wanamalizia vitu vidogo kabla ya kuanza kazi mwezi ujao.

"Mashine hizi zilizotolewa na serikali zitaanza kutumika mwezi ujao na zitatumika kwenye uchunguzi wa awali wa saratani na zitasaidia sana taasisi yetu katika kuwahudumia wananchi wanaofika hapa," alisema.

Dk. Mwaiselage aliishukuru serikali kwa jitihada zake za kudumisha utendaji kazi wa hospitali hiyo katika kuhudumia wananachi wanaofika kupata huduma.

Mkurugenzi huyo pia aliishukuru GBT kwa msaada iliotoa hospitalini huko wenye thamani ya Sh. milioni 40.

"Msaada huu utaenda kuwagusa moja kwa moja wagonjwa, hospitali yetu inapokea wagonjwa wengi sana na wengine wanaotoka nje ya Mkoa wa Dar es Salaam, wanakuwa hawajui hasa watakaa siku ngapi hospitalini, muda mwingine mahitaji yao wanayokuja nayo yanaisha kabla ya kuruhusiwa kutoka hospitalini.

"Misaada kama hii inawasaidia kuendelea kupata mahitaji yao muhimu wakiwa wodini," alisema Dk. Mwaiselage.

Akikabidhi misaada hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa GBT, James Mbalwe, alisema wametoa msaada huo katika kuadhimisha miaka 20 tangu bodi hiyo ianze shughuli zake rasmi.

"Misaada tunayokabidhi leo (juzi0 ina thamani ya Sh. milioni 25 pamoja fedha taslimu Sh. milioni 15 na kufanya thamani ya jumla kuwa Sh. milioni 40. Tumekabidhi makabati maalum ya wodini, pampers, sabuni, dawa za meno na maji, tunaamini zitasaidia," alisema Mbalwe.

# Aliyeua watu 16 kwa risasi asakwa

**WASHINGTON, Marekani**

POLISI nchini Marekani inaendelea na msako wa kumtafuta mtu aliyejihami kwa bunduki baada ya kufyatua risasi katika mitaa ya mji wa Lewiston ulioko jimbo la Maine nchini Marekani na kuua watu 16.

Mshukiwa wa shambulio hilo ametajwa kwa jina la Robert Card, ni mwalimu wa matumizi ya bunduki ambaye alifunzwa na jeshi la Marekani katika mji wa Saco, Maine, kulingana na taarifa ya polisi na kuonekana na shirika la Associated Press.

Taarifa hiyo ilisema kuwa mtu huyo alikuwa anatibiwa tatizo la akili katika kituo cha afya majira ya joto ya 2023 na alitishia kupiga risasi kwenye kituo hicho.

Ofisi ya Sherifu wa Kaunti ya Androscoggin, ilitoa picha mbili za mshukiwa, ikisema kuwa yuko katika makazi ya watu na kuomba usaidizi wa umma kumtambua.

Kwenye video zilizofanikiwa kunasa tukio hilo, ilionyesha mtu mwenye ndevu aliyevalia sweta ya kahawia akiwa amebeba bunduki akiingia kwenye jengo na kuanza kupiga risasi.

Polisi pia walishirikisha umma picha ya gari jeupe, wakisema bampa yake ya mbele inaaminika kuwa imepakwa rangi nyeusi, na kumtaka yeyote anayeitambua awasiliane na polisi.

Ikulu ya White House inasema Rais Biden amefahamishwa kuhusu hali ya Lewiston na ataendelea kupokea taarifa.

**BBC**

**Ofisi ya Sherifu wa Kaunti ya Androscoggin, ilitoa picha mbili za mshukiwa, ikisema kuwa yuko katika makazi ya watu na kuomba usaidizi wa umma kumtambua.**

MCB BANK BETTER TOGETHER

# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2023 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Septemba-2023 | Robo Mwaka iliyopita 30-Juni-2023 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 617 | 452 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 14,576 | 18,159 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 54 | 27 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 53 | 12 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 6,371 | 6,348 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 61,859 | 60,037 |
| 12. Mali Nyingine | 2,050 | 2,673 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 962 | 857 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **86,435** | **88,565** |
| **B. DHIMA:** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | 4,038 | 4,538 |
| 18. Amana za Wateja | 59,320 | 62,965 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,844 | 1,732 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 3,287 | 1,172 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27. Dhima Nyingine | 2,433 | 2,351 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **70,922** | **72,758** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **15,513** | **15,807** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30,912 | 30,912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | 17 | 17 |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (20,302) | (20,294) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (114) | 172 |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji (Mtaji tangulizi) | 5,000 | 5,000 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **15,513** | **15,807** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | | |
| 39. Mikopo Chechefu | 1,200 | 1,218 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | (592) | (461) |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 17.9% | 17.8% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.9% | 2.0% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 96.7% | 89.6% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 70.9% | 68.3% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 78.9% | 75.0% |
| - Ongezeko la Amana | -6.1% | 2.9% |
| - Ongezeko la Mali | -2.4% | 2.0% |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA 2023 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Septemba-2023 | Robo Mwaka iliyopita 30-Juni-2023 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Septemba-2023 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Septemba-2022 |
|---|---|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | (136) | 56 | (80) | 32 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - | - | - |
| - Hasara katika Mali | 496 | 309 | 805 | 932 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (5,408) | 3,563 | (1,845) | (21,602) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (2,903) | (742) | (3,645) | 21,337 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 73 | 2,236 | 2,309 | (1,196) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 2,544 | (1,527) | 1,017 | (1,033) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | (34) | - |
| - Mengineyo | 65 | 5 | 70 | (86) |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(5,268)** | **3,900** | **(1,402)** | **(1,616)** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| - Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | (120) | (89) | (209) | (223) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(120)** | **(89)** | **(209)** | **(223)** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | - | - | - | - |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | - | - | - | - |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | - | - | - | - |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu | (5,421) | 3,811 | (1,610) | (1,839) |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 10,845 | 7,034 | 12,727 | 6,051 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 5,424 | 10,845 | 11,117 | 4,212 |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2023 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Mtaji Tangulizi | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (20,254) | 5,000 | - | 15,658 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (114) | | - | (114) |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | - | | 17 | 17 |
| Mengineyo | - | (48) | | - | (48) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(20,417)** | **5,000** | **17** | **15,513** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (19,895) | 5,000 | - | 16,017 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | (331) | | | 331 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | (17) | | 17 | - |
| Mengineyo | - | (11) | | - | (11) |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(20,254)** | **5,000** | **17** | **15,675** |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2023 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo ya Mwaka sasa 30-Septemba-2023 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Setemba-2022 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Septemba-2023 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Septemba-2022 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 2,524 | 2,280 | 7,711 | 6,103 |
| 2. Gharama za Riba | 1,295 | 847 | 3,387 | 2,313 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **1,229** | **1,433** | **4,324** | **3,790** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 126 | - | 206 | - |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 454 | 492 | 1,332 | 1,516 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | (9) | - | (8) | 4 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 431 | 464 | 1,159 | 1,404 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 32 | 28 | 181 | 108 |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 1,843 | 1,899 | 5,530 | 5,273 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 760 | 788 | 2,377 | 2,355 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 1,083 | 1,111 | 3,153 | 2,918 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **(286)** | **26** | **(80)** | **32** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | - | (6) | (34) | (6) |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **(286)** | **20** | **(114)** | **26** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(286)** | **20** | **(114)** | **26** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 67 | 61 | 67 | 61 |
| 14. Mapato kwa Hisa | -5 | 0 | -1 | 0.5 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | *-0.3%* | *0.0%* | *-0.1%* | *0.0%* |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | *-1.9%* | *0.13%* | *-0.7%* | *0.16%* |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo na Riba na Mapato Ghafi | *109.5%* | *98.6%* | *97.8%* | *99.4%* |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | *1.8%* | *2.1%* | *6.3%* | *5.6%* |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2023**

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha za robo, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Richard L. Makungwa (Ofisa Mtendaji Mkuu) | ......................... (Imesainiwa) | 20 Oktoba 2023 |
| Maulid M. Tarimo (Kaimu Mkuu wa Fedha) | ......................... (Imesainiwa) | 20 Oktoba 2023 |
| Joanitha Mashulano (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ......................... (Imesainiwa) | 20 Oktoba 2023 |

**Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1/ Francis Ramadhani (Mwenyekiti) | ......................... (Imesainiwa) | 20 Oktoba 2023 |
| 2/ Kissa Kilindu (Mkurugenzi) | ......................... (Imesainiwa) | 20 Oktoba 2023 |

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES MADE UNDER REGULATION 11

| S/N. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| 1 | **Current Accounts** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 50,000 |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer | TZS 7,500 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 2,500 for amounts less than 5Mil otherwise 0.1% max TZS 100,000 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | TZS 1,300 |
| | (e) ATM mini statement | TZS 300 |
| | (f) Interim statement per page | TZS 1,500 |
| | (g) Periodic scheduled statement | 0 |
| | (h) Cheque book | TZS 500 per leaf |
| | (i) Dishonoured cheque | TZS 100,000 |
| | (j) Special clearance | n/a |
| | (k) Counter cheque | TZS 6,000 |
| | (l) Stop payment | TZS 40,000 |
| | (m) Standing order (Same bank) | Free |
| | (n) Balance enquiry | TZS 300 |
| | (o) New ATM card issuance | TZS 10,000 |
| | (p) ATM card renewal or replacement (indicate costs for different card types) | TZS 10,000 |
| | (q) Overdrawn account interest charge | 20% |
| | (r) Unarranged overdraft | 20% |
| | (s) Interbank transfer | TZS 10,000 |
| | (t) Bill payments through ATM | n/a |
| | (u) Deposit fee | 0 |
| | (v) Other (please specify) | n/a |
| 2 | **Savings Accounts (Disclose for product specifictypes)** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 5,000 |
| | (b) Monthly service fee | TZS 1,400 |
| | (c) Interim statement | TZS 1,500 |
| | (d) Account closure | TZS 20,000 |
| 3 | **Electronic Banking** | |
| | (a) Internet banking monthly fee | n/a |
| | (b) Internet transfers | n/a |
| | (c) SMS banking | TZS 1700 |
| | (d) Other | n/a |
| 4 | **Foreign Exchange Transaction** | |
| | (a) Purchase/sale of TCs transactions over the | n/a |
| | (b) Purchase of foreign cheque | n/a |
| | (c) Sale/purchase of cash passport | n/a |
| | (d) Telegraphic transfer | n/a |
| | (e) Telex/SWIFT | n/a |
| | (f) Tranfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank) | 0 |
| 5 | **Personal Loans** | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | 0.77% p.a |
| | (i) Personal loans | 16% |
| | (ii) Overdrafts | 20% |
| | (iii) Mortgage finance | n/a |
| | (iv) Asset finance | n/a |
| | (b) Unpaid loan instalment | 20% |
| | (d) Valuation fees | n/a |
| | (e) Other | n/a |

**Deposit Rates**

| | Fixed Deposit - TZS | 3 Months | 6 Months | 12 Months |
|---|---|---|---|---|
| | 1 - 2 Mln | 1.5% | 2.0% | 2.5% |
| | 2 - 10Mln | 2.0% | 2.5% | 3.0% |
| | 10 - 50 Mln | 2.5% | 3.0% | 3.5% |
| | 50 - 100 Mln | 3.0% | 3.5% | 4.0% |
| | 100 - 300 Mln | 3.5% | 4.0% | 4.5% |
| | 300 - 500 Mln | 4.0% | 4.5% | 5.0% |
| | 500m - 1Bln | 4.5% | 5.0% | 5.5% |
| | Above 1 Bln | Contact Treasury | | |
| | **Savings Account - TZS** | **Accrue on Daily Cleared balance paid Monthly** | | |
| | 0- 50k | 0.5% | | |
| | 50k - 1mln | 1.0% | | |
| | 1 - 10mln | 1.5% | | |
| | 10 - 100mln | 2.0% | | |
| | Over 1mln | 2.5% | | |

**Base Lending Rates**

| | Loan Type | Base rate | |
|---|---|---|---|
| 1 | Short term (up to 1year) | 19.5% | +/-4.5% |
| 2 | Medium term (2-4 years) | 21.5% | +/-1.5% |
| 4 | Term loans (over 5 years) | 19.0% | +/-4.0% |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Richard L. Makungwa | Chief Executive Officer | | 20 October 2023 |
| 2 | Leticia Ndongole | Head of Business Development & Marketing | | 20 October 2023 |
| 3 | Maulid M. Tarimo | Ag Head of Finance | | 20 October 2023 |

217672602

## ZISIKUPITE

**DE GEA KUREJEA**

KLABU ya Manchester United itabadili msimamo na kumtaka David de Gea arejee kwa mkataba wa muda mfupi ikiwa ni miezi minne tu baada ya kumruhusu mlinda mlango huyo wa zamani wa Hispania mwenye umri wa miaka 32, kuondoka mwishoni mwa mkataba wake. **(Sun)**

**MUSIALA ATAKIWA CITY**

KLABU ya Manchester City inachunguza uwezekano wa kumsajili winga wa Bayern Munich, Jamal Musiala mwenye umri wa miaka 20. **(Sport)**

**PALHINHA HAIJULIKANI**

BAYERN Munich haina uhakika kuhusu kutafuta ofa ya kumnunua Joao Palhinha wa Fulham Januari baada ya kukaribia kumsajili kiungo huyo wa kati wa Ureno mwenye umri wa miaka 28, msimu uliopita. **(Bild)**

**NORMAND AWINDWA**

MANCHESTER United na Liverpool zimekuwa zikimtazama beki wa Hispania Robin le Normand mwenye umri wa miaka 26, na wanaweza kumsajili kutoka Real Sociedad mwaka ujao. **(Team Talks)**

**MOLINA ATAKIWA VILLA**

KLABU ya Aston Villa imeibuka kuwa mstari wa mbele kumsajili beki wa kulia wa Atletico Madrid, Nahuel Molina mwenye umri wa miaka 25 ambaye aliisaidia Argentina kushinda Kombe la Dunia mwaka jana. **(Fichajes)**

**MOURINHO KUONDOKA**

KOCHA wa Ureno, Jose Mourinho anatarajiwa kuondoka AS Roma mwishoni mwa msimu huu na mshambuliaji wa England, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 26 anaweza kumfuata.**(Team Talks)**

**CACERES KUSAJILIWA WEST HAM**

KLABU ya West Ham inaweza kukamilisha usajili wa beki wa kati wa Club America na Uruguay, Sebastian Caceres mwenye umri wa miaka 24 Januari kwa kitita cha paumi milioni 6. **(Football Insider)**

**UNITED, CITY ZAMFUATILIA KAYODE**

KLABU za Manchester United, Arsenal na Manchester City zinaendelea kumfuatilia Michael Kayode licha ya beki huyo wa kulia wa Italia mwenye umri wa miaka 19 kutia saini mkataba mpya Fiorentina. **(90min)**

**MAATSEN KUONDOKA CHELSEA**

IAN Maatsen anatarajiwa kuondoka Chelsea Januari mwakani baada ya kushindwa kupata nafasi ya kuanza, lakini Mholanzi huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye anacheza nafasi ya beki wa kushoto au kiungo, hana nia ya kurejea Burnley ambako alikaa msimu uliopita kwa mkopo. **(Team Talks)**

**MRITHI WA MOYES ATAFUTWA**

KLABU ya West Ham iko tayari kuanza kutafuta mbadala wa kocha wake wa sasa, David Moyes. **(Football Insider)**

**SOKRATIS KUMFUATA BELLERIN**

BEKI wa zamani wa Ugiriki, Sokratis Papastathopoulos mwenye umri wa miaka 35, anatazamiwa kuungana tena na mchezaji mwenzake wa zamani wa Arsenal, Hector Bellerin huko Real Betis akiwa mchezaji huru tangu aondoke Olympiakos. **(Fabrizio Romano)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MANÉ KUNUNUA KLABU UFARANSA

- Anafikiriwa zaidi kuwekeza kwenye klabu hiyo inayoshiriki Ligi daraja la...

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Senegal, Sadio Mané yuko katika harakati za kuinunua klabu ya daraja la nne ya Ufaransa Bourges Foot 18, kwa mujibu wa ESPN.

Mané mwenye umri wa miaka 31, anafikiriwa kuwa tayari kuwekeza katika klabu ya soka kwa muda na uhusiano wake na rais wa zamani wa Bourges Foot 18 Cheikh Sylla ulikuwa muhimu katika uwekezaji wake.

Chanzo kimoja kiliiambia ESPN kwamba Mané alichangia baadhi ya fedha kwa klabu ili kuwasaidia katika kuajiri wachezaji wakati wa dirisha la lililopita la usajili la majira ya joto, lakini tangazo la Jumatano litamfanya mchezaji huyo wa zamani wa Liverpool na Bayern Munich kuwa mmoja wa wawekezaji.


Ununuzi wa Mané pia umepokelewa na idhini ya meya wa jiji, Yann Galut.

Klabu hiyo iliyo umbali wa kilomita 250 kutoka Paris katikati mwa Ufaransa haijawahi kucheza zaidi ya ligi ya daraja la pili ya Ufaransa. Bourges wanashika nafasi ya pili katika Kundi B katika Ligi ya Taifa.

Mane alisajiliwa na klabu ya Al Nassr inayoshiriki Ligi ya Saudia Agosti Mosi mwaka huu baada ya mwaka mgumu akiwa Bayern ambao ulipelekea kusimamishwa na klabu hiyo baada ya kudaiwa kuzozana na mchezaji mwenzake Leroy Sané kufuatia kushindwa kwa timu hiyo kwenye Ligi ya Mabingwa dhidi ya Manchester City.

Mané alishinda mataji sita wakati alipokuwa Anfield, ikiwa ni pamoja na Ligi ya Mabingwa mwaka 2019 na Ligi Kuu ya 2020.

# HOJLUND AKATAA KUFANANISHWA NA HAALAND



**MANCHESTER, England**

RASMUS Hojlund amesisitiza kuwa hataki kulinganishwa na Erling Haaland huku wawili hao wakijiandaa kumenyana katika mchezo wa Manchester dabi Jumapili.

Hojlund ameanza vyema tangu alipohamia Manchester United kwa pauni milioni 64, akiwa amefunga mabao matatu katika mechi tatu za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Asili ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark na mtindo wake wa kucheza umesababisha kulinganishwa na mchezaji wa Manchester City, raia wa Norway, Haaland.

Lakini Hojlund mwenye umri wa miaka 20, analenga katika kujenga sifa yake mwenyewe huku akijinadi kutafuta miguu yake kwenye Ligi Kuu.

Katika matokeo ya ushindi wa 1-0 wa United dhidi ya klabu ya zamani ya Hojlund, FC Copenhagen juzi usiku, alisema, "Kama nilivyosema mara nyingi. Sitaki kulinganishwa naye.

"Yeye ni mzuri na pengine ndiye mshambuliaji bora zaidi duniani. Natumaini anaweza kuimarika kisha tutaona kitakachotokea," alisema Hojlund na kuongeza,

"Itakuwa uzoefu mkubwa kucheza dhidi yake. Ninasubiri kwa hamu, siku zote ni maalum kucheza na mpinzani. Ikiwa tutashinda mchezo, tunaweza kukaribia kileleni."

Licha ya kushindwa kufunga katika mashindano ya ndani tangu ajiunge na United, Hojlund ana imani kwamba kuna mengi zaidi yajayo.

"Nimejaribu kufanya vyema kila ninapocheza lakini bado mambo hayako sawa, tumekuwa tukihangaika kidogo lakini tunafika sasa, tumeshinda mara tatu mfululizo. Kila mchezo wa Ligi Kuu unakufanya unazoea ligi zaidi.

"Ninaimarika kila siku na wachezaji wenzangu wameanza kuona mifumo yangu kwenye mchezo pia, hivyo inazidi kuwa bora.

"Ninajua lazima nifanye maonyesho kila siku. Lakini mwisho wa siku, nina umri wa miaka 20 tu bado nina mengi ya kuboresha lakini tutaendelea." alisema nyota huyo.

# Pulisic anaamini Milan bado ina nafasi

**MILAN, Italia**

NYOTA wa AC Milan, Christian Pulisic amesema anaamini timu hiyo bado ina nafasi ya kufanya vizuri katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya licha ya kufungwa mabao 3-0 na PSG Juzi Jumatano na kuwaacha wababe hao wa Italia wakiwa mkiani mwa Kundi F.

Milan wana pointi mbili pekee katika michezo yao mitatu ya kwanza waliyocheza katika kundi lao ambalo linaaminika kuwa gumu zaidi katika mashindano ya msimu huu.

Pia bado hawajafunga bao, baada ya kutoka sare tasa nyumbani dhidi ya Newcastle United na Borussia Dortmund kabla ya kufungwa Jumatano katika mji mkuu wa Ufaransa.

"Lazima tuangazie mchezo unaofuata. Bado hatujatoka, tunahitaji tu kuunganisha nguvu pamoja," alisema Pulisic akiiambia CBS Sports.

"Tumekuwa na michezo migumu katika baadhi ya viwanja vigumu lakini hicho sio kisingizio, tunahitaji kugeuza na tunahitaji kushinda."

Washambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe na Randal Kolo Muani walifunga mapema na kuifanya PSG kutawala uwanjani wa Parc des Princes kabla ya winga wa Korea Kusini, Lee Kang-in kuongeza bao la tatu dakika za mwisho.

Milan walipata nafasi nzuri ya kusawazisha bao muda mfupi baada ya kipindi cha mapumziko Pulisic alipokimbia nje




ya eneo la hatari lakini badala ya kupiga shuti mwenyewe, aliamua kumpasia Olivier Giroud, ambaye shuti lake lilipaa juu ya lango.

"Hatukuwa na nguvu ya kutosha, ni juu yetu, lazima tuendelee kufanya kazi na kupambana, nadhani inabidi tuweke vichwa vyetu juu. Hatukupaswa kupoteza 3-0, huu ni ujumbe.

"Tutakuwa sawa kwenda mbele, sisi ni kundi la watu wanaojiamini, jambo zuri la ratiba hii ni kwamba tuna mchezo mwingine ndani ya siku chache," alisema nyota huyo.

Pulisic alisajiliwa na Milan msimu uliopita wa joto kutoka Chelsea na akajiunga na mchezaji mwenzake wa Marekani, Yunus Musah.

Wawili hao wameisaidia Milan kuanza vyema msimu huu nyumbani, wakiwa nyuma kwa pointi moja dhidi ya viongozi wa Serie A, Inter Milan baada ya mechi tisa.

Lakini ikiwa Milan wanataka kutinga hatua ya mtoano ya Ligi ya Mabingwa wakiwa miongoni mwa timu mbili za juu katika kundi, huenda wakahitaji matokeo chanya watakapoikaribisha PSG kwenye Uwanja wa San Siro katika muda wa wiki mbili zijazo.

"Kila mpinzani ni tofauti, kila mpinzani ni timu ya juu," Musah aliwaambia wanahabari. "Kila mtu anazungumzia jinsi kundi letu lilivyo na ugumu, kwa hivyo tunapaswa kuzidisha tena kiwango wakati tutakapocheza nao.

"Haikuwa ngumu kwetu tu, ilikuwa ngumu kwao pia. Tuliwaweka chini ya shinikizo, tulifanya wafanye makosa, tulitengeneza nafasi kadhaa lakini walituadhibu na hatukufanya hivyo," alisema.

# Roma yapigwa rungu Serie A

**ROME, Italia**

AS Roma imepigwa faini ya euro 10,000 na Serie A baada ya waokota mipira wao kuchelewesha mchezo kwa makusudi Jumapili dhidi ya Monza.

Katika mchezo huo, vijana wa Jose Mourinho walipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Monza shukrani kwa bao la Stephan El Shaarawy dakika ya 90.

Bodi ya Ligi ya Italia aliamua kwamba waokota mpira wa Roma walichukua muda mwingi kurudisha mpira baada ya wenyeji kufunga bao la ushindi.

Taarifa ya ligi ilisomeka, "Roma wanawajibika kwa vijana wao wa kuokota mpira kuchelewesha kwa makusudi kuanza tena kwa mchezo, na kulazimisha mwamuzi kuongeza muda wa kwa dakika mbili."

Mourinho pia alilimwa kadi nyekundu na atakosa mchezo mmoja.

Akiwa na kadi nyekundu, Mourinho hatakuwa kwenye benchi katika mechi inayofuata ya ligi ya Roma ugenini dhidi ya klabu yake ya zamani Inter Milan.

Kocha huyo raia wa Ureno alizungumza siku za nyuma kuhusu waokota mipira.

Wakati alipokuwa Tottenham Hotspur, Mourinho alimsifu mvulana wa klabu kwa kuurusha mpira kwa haraka kwa Sèrge Aurier ambao ulisababisha bao la kusawazisha katika ushindi wa 4-2 wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Olympiakos.

"Ninawapenda waokota mpira wenye akili, kama nilivyokuwa," alisema Mourinho wakati huo.

"Nilikuwa mvulana mzuri sana kama mtoto. Mtoto huyu leo alikuwa na kipaji. Anasoma mchezo, anaelewa mchezo na alitoa pasi muhimu."



HABARI MICHEZO

# BASENA AIHOFIA SIMBA

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Ihefu FC, Mosses Basena amekitazama kikosi cha Simba na kukiri ana kazi kubwa ya kufanya katika kutafuta matokeo mazuri kwenye mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Jumapili ijayo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa saa 1:00 jioni.

Akizungumza na Nipashe jana, Basena alisema wamejiandaa vizuri kuwakabili wenyeji wao hao licha ya mchezo huo kuwa na ushindani mkubwa kwa sababu ya ubora wa Simba.

Alisema wanahitaji kupata matokeo mazuri na amewaangalia vizuri Simba ameona ubora wa mchezaji mmoja mmoja na ubora wao mkuba kwenye safu ya ushambuliaji.

"Nafahamu mpira wa Simba , nimewaona walivyocheza mechi zote mbili za African Football League (AFL ) dhidi ya Al Ahly ya Misri, tumeona ubora wao na kufanyia kazi madhaifu yetu ili kutafuta matokeo chanya Jumamosi," alisema Basena na kuongezea,

"Mchezo wa mpira wa miguu ni dakika 90 ambazo ndizo zinatoa maamuzi na kapata nini, kikubwa naandaa timu kwa ajili ya mchezo mzuri naamini itakuwa mechi ya kimbinu na kiufundi kwa sababu ya aina ya mpira tutakaocheza," alisema Basena.

Aliongeza kuwa wataenda kucheza mchezo huo kwa nidhamu ya hali ya juu hasa safu yake ya ulizi kuwaheshimu wapinzani kutokana na ubora wa safu ya ushambuliaji wa Simba .

Safu ya ushambuliaji wa Simba inaongozwa na Nahodha John Bocco, Mosses Phiri na Jean Baleke ambaye ni kinara wa kufumania nyavu ndani ya kikosi cha Wekundu hao wa Msimbazi akiwa na mabao matano.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa COSOTA, Doreen Sinare (wa pili kushoto) akiwa na Mkurugenzi wa Kampuni ya Art & Home, Aminiel Lukumay (katikati ) wakati wa uzinduzi wa maonyesho ya Sanaa jijini Dar es Salaam jana, wengine ni wadau mbalimbali wa sanaa.**PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Ibra Class awaita mashabiki PTA

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA wa ngumi za kulipwa nchini Ibra Class amesema yupo tayari kwa pambano lake la leo dhidi ya Xiao Tao Su kutoka China na amewataka mashabiki wa ngumi kujitokeza kwa wingi kwenye ukumbi wa PTA jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Class alisema licha ya kutomfahamu vizuri mpinzani wake huyo, hana wasi wasi kutokana na maandalizi ya muda mrefu aliyoyafanya.



"Sijawahi kuona pambano lake lolote wala simfahamu, nitakutana naye siku ya pambano kwa mazoezi niliyoyafanya ninaamini nitafanya vizuri," alisema Class.

Alisema amerejea jijini Dar es Salaam juzi akitokea Tanga alipokuwa ameweka kambi chini ya Kocha wake Hamis Mwakinyo.

Alisema kambi hiyo itamsaidia kwa kiasi kikubwa kutoa burudani kwa mashabiki wake pamoja na watanzania kwa ujumla.

"Lengo langu ni kupata ushindi katika pambano la kesho (leo), najua halitakuwa pambano jepesi lakini niwatoe mashabiki wanguna wapenzi wa ngumi, nimejiandaa vizuri sana na sitawaangusha," alisema Class.

Amewataka mashabiki kujitokeza kwa wingi kumpa sapoti na kushuhudia akimpiga mpinzani wake huyo.

# TGU, NCBA wazindua mashindano ya Gofu

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Mchezo wa Gofu Tanzania (TGU) kwa kushirikiana na benki ya NCBA kimezindua mashindano ya mchezo huo yatakayofanyika jijini Arusha.

Mashindano hayo yakayofanyikia kwenye viwanja vya Gofu vya Kilimanjaro mkoani humo yamepangwa kuanza Novemba 23 mpaka 26.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa mashindano hayo jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa TGU, Gilman Kasiga alisema chama hicho kinawashukuru wadhamini wao NCBA kwa kukubali kushirikiana kuanzisha mashindano hayo mkoani.

"Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa benki hii kwa hapa Tanzania, naamini mashindano haya yatakuwa yenye upinzani mkubwa, wachezaji mbalimbali kutoka mikoa tofauti watashiriki," alisema Kasiga.

Alisema ushiriki wa NCBA katika mashindano hayo utachochea makampuni na taasisi nyingine kujitokeza kudhamini mashindano mengine yanayoandaliwa na TGU.

# Serikali kuendelea kuunga mkono Sanaa

**Na Mwandishi Wetu**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Haki Miliki Tanzania (COSOTA), Doreen Sinare, amesema kuwa Serikali itaendelea kuunga mkono shughuli za kiuchumi kupitia sanaa zinazofanywa na watanzania hapa nchini.

Hayo ameyasema jana jijini Dar es Salaam alipokuwa akifungua maonesho ya bidhaa mbalimbali za Sanaa ya ufundi nchini.

"Nimetembelea maonesho ya bidhaa zinazotokana na Sanaa za ufundi zilizotengenezwa na vikundi, watu binafsi, kampuni za ndani na nje ya nchi ama kwa hakika nimeguswa mno na bidhaa zenye ubora na zinazovutia, ahadi yangu kwenu na kwa niaba ya Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma aliyetakiwa kuwa mgeni rasmi niseme kwamba Serikali itaendelea kushirikiana nanyi katika mnyororo wa thamani wa kazi za sanaa za fundi" alisema Doreen

Afisa Mkuu huyo alitanabaisha wazi kwamba endapo wananchi watachangamkia fursa zilizopo katika bidhaa za Sanaa za ufundi watauaga umaskini kwakuwa ipo biashara kubwa ndani yake.

"Kama wananchi hususani wasanii watatumia vizuri fursa hii wanaweza kutengeza fedha nyingi kupitia saa zao, kama Serikali tutaendelea kuwajengea mazingira mazuri ya kuwafanya wanufaike na sanaa zao," alisema Doreen.

Maonyesho hayo yaliandaliwa nja kampuni ya Art &Home ambapo Mkurugenzi wake Aminiel Lukumay alisema sababu kubwa ya kuandaa maonesho hayo ni shauku waliyonayo ya kuhakikisha Sanaa za ufundi hususani wa majumbani zinapewa kipaumbele.

"Tumezoe kununua bidhaa nyingi,nzuri na bora za majumbani pasipokuwafahamu watengenezaji na waagizaji aidha kutoka nje au ndani ya nchi zaidi ya kuziona sokoni, kwa hiyo sisi kwa kushirikiana na wenzetu tumeamua kufanya maonesho haya katika wiki hii ya siku ya Sanaa duniani ili kuwaunganisha walaji wa bidhaa za Sanaa za ufundi na wasanii wenyewe",alisema Lukumay.

# Michezo

Ijumaa Oktoba 27, 2023
Nipashe




**Mané kununua klabu Ufaransa** UKURASA 21



Mshambuliaji wa Twiga Stars, Aisha Masaka (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa Botswana katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki Michezo ya Olimpiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana, Stars ilishinda bao 2-0. Timu hizo zitarudiana tena Oktoba 31, mwaka huu jijini Gaborone. **PICHA: TFF**

# YANGA KUITUMIA SINGIDA FG KUJIIMARISHA KILELENI LEO

## ●●●Inawakabili Singida FG huku Gamondi akitabiri kuwa ugumu katika mchezo wa leo unatokana na...

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Yanga, Miguel Gamondi amesema kuwa mchezo wao wa leo dhidi ya Singida Fountain Gate hautakuwa mwepesi kutokana na kuimarika kwa wapinzani wao, hata hivyo wanataka kujiimarisha kileleni kwa kusaka ushindi.

Gamondi, amesema wapinzani wao hao wamezidi kuimarika hivyo wanatarajia upinzani mkubwa kutoka kwao kwenye mchezo wa leo utakaochezwa saa 12:00 jioni.

"Lakini lazima tupiganie malengo yetu, tunataka kuendelea kukusanya pointi ya kubaki kileleni, tunajua mchezo utakuwa wa upinzani mkubwa, muhimu kwetu ni pointi tatu," alisema Gamondi na kuongezea,

"Nimewaona kwenye michezo mbalimbali ya Ligi Kuu pamoja na Kombe la Shirikisho Barani Afrika naamini utakuwa mchezo mgumu maana tumekuwa tukicheza michezo mfululizo na wao wameimarika zaidi," alisema Gamondi.

Kwa upande wake, Kocha wa Singida Fountain Gate, Ricardo Ferreira alisema baada ya mechi na Namungo FC walifanya maandalizi mazuri na kufanyia kazi mapungufu waliyoyaona tayari kwa mchezo wa leo. "Tumefanikiwa kuona baadhi ya mechi za Yanga, hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu kila mmoja anahitaji alama tatu, tutacheza kwa nidhamu kubwa ili kutumia mapungufu ya wapinzani wetu kutafuta matokeo mazuri," alisema Ferreira.

Katika michezo mingine inayopigwa leo Azam FC itacheza na Namungo kwenye uwanja wa Azam Complex huku KMC ikiwakaribisha Tanzania Prisons kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, mchezo huo utaanza saa 10:00 jioni

Kuelekea mchezo wake, Kocha wa Azam FC, Bruno Ferry alisema baada ya kupoteza mechi yao dhidi ya Yanga walirejea kwenye uwanja wa mazoezi na kufanyia kazi kile alichokiona hakikwenda sawa kwenye mchezo huo.

"Kikosi kipo tayari, kazi tumemaliza kilichobaki ni muda wachezaji kufanya kazi yao ya kutafuta alama tatu muhimu katika mchezo huo. Ni muhimu kushinda ili kuendelea kujiweka kwenye mazingira mazuri ya mipango yetu ya kuwania nafasi tatu za juu," alisema Ferry.

Kocha Msaidizi wa Namungo FC, Denis Kitambi alisema wanajua mazingira waliyopo sio mazuri na mkakati ni kuungana ili kujinasua kwenye eneo waliopo sasa katika msimamo wa ligi.

"Utakua mchezo mgumu lakini tumejipanga kupata ushindi tunajua Azam ni timu kubwa lakini tumejipanga kupambana nao, fikra zetu ni kuondoka tulipo sasa kwenye msimamo, tuna mechi 24 mbele yetu hivyo tunataka kubadili kile kilichopita, mashabiki wasikate tamaa waendelee kutuunga mkono," alisema Kitambi.

## Robertinho aelekeza nguvu ligi kuu

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuondolewa kwenye michuano ya African Football League, kocha wa Simba Robert Oliviera 'Robertinho' amesema sasa wanaelekeza nguvu kwenye michezo yao ya ligi kuu na ameanza kufanyia kazi mapungufu aliyoyaona kwenye kikosi chake.

Kocha huyo raia wa Brazil, alisema kwa sasa muhimu ni kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye michezo yao ya ligi kuu kabla ya kuanza 'heka heka' ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo timu hiyo ipo kwenye kundi C hatua ya makundi ya michuano hiyo.

"Yapo maeneo kama nilivyosema tumeanza kuyafanyia kazi kukiimarisha zaidi kikosi chetu, kwa sasa akili yetu yote ipo kwenye michezo inayokuja ya ligi kuu, hatujapoteza mchezo mpaka sasa , na tunataka kuendelea hivyo," alisema Robertinho.

Alisema, mchezo wao unaofuata wa ligi kuu dhidi ya Ihefu ni muhimu zaidi kwao kupata ushindi hili kuendeleza morali ya wachezaji wake na kuendeleza furaha za mashabiki wao ambao wamekuwa wakiwasapoti siku zote.

"Nichukue pia nafasi hii kuwashukuru sana mashabiki wetu, wamekuwa na msaada mkubwa kwetu kwa sapoti yao, tunataka tushinde mchezo wetu unaofuata ili kuendeleza furaha kwao kama asante yetu kwa sapoti yao kwetu," alisema Robertinho.

Alisema anajivunia zaidi kikosi chake ambacho wachezaji wake wamekuwa wakifuata maelekezo yake kwenye mechi kulingana na mpinzani tunayekutana naye na hilo limekuwa jambo bora kwao.

Simba inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 15 baada ya kucheza michezo mitano ikizidiwa kwa idadi ya mabao ya kufunga na wapinzani wao Yanga wanaoshika nafasi ya kwanza kwenye msimamo, hata hivyo Yanga watakuwa na michezo miwili zaidi baada ya mchezo wao wa leo dhidi ya Singida Fountain Gate.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >